SUPA JACKPOT
TZS.1,096,041,286
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Mwinyi**: Asitokee kiongozi kuwatisha watoa taarifa

UKURASA 4



ama
AFYA NA MAZINGIRA
Waguzi wakiri kuna 'vishoka' kati yao, waamua kupambana nao
Wanamazingira wathibitisha uwezekano kurejeshea Milima Uluguru kijani cha misitu
Rais katika miaka miwili akibeba ushuhuda wa kukomboa mtoto
KUTOKA DODOSO LA KILELE...
Miaka miwili Awamu ya Sita, wiki iliyosheheni uzinduzi miradi maji

UKURASA 11

Nipashe
Alhamisi Machi 30, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581265
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

## RIPOTI YA CAG

# Madudu tena

UKURASA 2



**Hasara mradi wa SGR sababu za kimkataba**




**Mabilioni yalipwa nje ya mkataba Bwawa la Mwalimu Nyerere**




**Upungufu ukusanyaji mapato TRA, upigaji fedha halmashauri**



**Ufanisi mdogo TPA kutokana na udhaifu wa mifumo**



**Baadhi ya visima havitoi maji licha ya kukabidhiwa kwenye mamlaka**

## SAUT sasa kurejesha shahada za madaktari 162

UKURASA 4



Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea taarifa ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2021/2022 kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Charles Kichere, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## ...Rais ataka waliohusika wawajibishwe, mashirika mizigo kwa serikali yafutwe

UKURASA 2&3

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA SC KAZI IENDELEE** UK.24 **KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea taarifa ya Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) kwa mwaka 2021/2022 kutoka kwa Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, CP Salum Hamduni, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Madudu tena ripoti CAG, TAKUKURU

**Na Jenifer Gilla**

NI madudu tena. Ndivyo inavyoweza kusemwa baada ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa mwaka wa fedha 2021/22 kuonyesha madudu katika sekta na taasisi mbalimbali za serikalini zikiwamo maji, Bwawa la Mwalimu Nyerere na Shirika la Reli Tanzania (TRA).

Madudu kama hayo yamekuwa yakijirudia kila mwaka kwenye ripoti za ukaguzi na kuonekana kuwa ni jambo la kawaida.

Akiwasilisha ripoti jana, Ikulu jijini Dar es Salaam kwa Rais Samia Suluhu Hassan, CAG Charles Kichere alisema katika maeneo mengi kumebainika upungufu zikiwamo kasoro katika utekelezaji wa mradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ya maji.

CAG alisema katika uboreshaji na usambazaji wa maji Same-Mwanga -Korogwe wenye thamani ya Sh. bilioni 263.5 kwa ufadhili wa serikali ya Tanzania na washirika wa maendeleo, ulioanza Desemba 17, 2014 na ulitakiwa ukamilike Machi 4, 2021 lakini hadi sasa haujakamilika.

Alisema makandarasi wawili waliingia mikataba mitatu kutekeleza mradi huo lakini yote ilisitishwa Desemba 2020, mikataba miwili ikisitishwa baada ya Wizara ya Fedha na Mipango kujiridhisha kuwa mkandarasi alighushi dhamana ya benki ya malipo ya awali pamoja na dhamana za fedha za zuio.

Kwa mujibu wa Kichere, mkataba mmoja ulisitishwa baada ya mkandarasi kutohuisha dhamana ya utekelezaji wake baada ya muda kuisha, kisha wizara ikaingia mikataba mingine miwili ya Dola za Marekani milioni 17.56 (Sh. bilioni 41.085) kwa ajili ya kusambaza mabomba na matangi bila ya kufunga mkataba wa awali.

"Kabla mkandarasi mpya hajaanza kazi Wizara ya Maji ilifanya mabadiliko (variation order) namba moja kwenye mkataba wa kujenga matangi, hivyo kuongeza gharama za mkataba kutoka Dola za Marekani milioni 3.61 hadi Dola milioni 5.9 sawa na ongezeko la asilimia 61," alisema.

Pia alisema walifanya ukaguzi wa ufanisi wa uendeshaji katika matengenezo ya usambazi wa maji na kugundua mamlaka tatu kati ya nne hazikuwa na utaratibu rasmi unaojitosheleza katika kuandaa mipango, ratiba na taratibu za kuongoza waendesha miundombinu ya maji iliyopo kwenye maeneo yao.

Alitolea mfano Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi huku akibainisha kuwa visima vinne kati ya vinane vya maji katika mradi wa Ng'apa vyenye uwezo wa kuzalisha maji lita ujazo 2,859 kwa siku vilikuwa havifanyi kazi.

Aidha, alisema kumekuwa na upotevu wa maji asilimia 20 kwa mwaka wa fedha 2019/20, 2020/21 na 2021/22 katika mamlaka nane zilizokaguliwa kutokana na wizi wa maji, kupasuka mabomba, mita za maji kutokusoma kwa usahihi na usanifu mbaya hatua iliyosababisha kupotea Sh. bilioni 57.2 kwa mwaka wa fedha 2019/20 na Sh. bilioni 60.94 mwaka 2020/21.

**HASARA MASHIRIKA**

CAG alisema mashirika 14 ya kibiashara yalipata hasara mwaka 2020 hadi 2022 likiwamo TRC ambalo mwaka 2020/2021 lilipata hasara ya Sh. bilioni 22.872 huku mwaka 2021/22 likipata hasara ya Sh. 31.295 hali inayoathiri mitaji iliyowekwa na serikali.

Alisema alisema shirika hilo lilikataa zabuni mara mbili kwa ajili ya ununuzi wa vichwa vya treni ya umeme na makochi ya abiria na mzabuni aliye na bei ya chini alikuwa na Dola za Marekani milioni 263.4, hivyo kufanya ununuzi usio wa ushindani wa Dola milioni 478.5. Hatua hiyo, alisema ilisababisha ongezeko lisilo la lazima la Dola za Marekani milioni 215.4 sawa na asilimia 82.

Kichere alisema pia shirika hilo lilitekeleza mkataba wa treni ya kawaida na makochi ya abiria bila dhamana ya utendaji, hali iliyosababisha hasara ya Sh. bilioni 13.7 kutokana na mkandarasi kushindwa kutekeleza mkataba na TRC kushindwa kutoza gharama zinazotokana na uvunjifu wa masharti hayo.

Mbali na TRC, alisema Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) liliongeza muda wa mkandarasi katika mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere hadi Juni 18, 2023 kutokana na makadirio yasiyo halisi na kasi ndogo ya utekelezaji.

Alisema mkandarasi anahitaji afikie asilimia 2.92 ya utekelezaji kila mwezi lakini kutokana na ucheleweshaji wa siku 15 hadi 155, inaonyesha kuwa mradi utakamilika Oktoba 2024 zaidi ya muda ulioongezwa.

# Samia ataka mashirika mzigo serikalini yafutwe

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema umefika wakati wa kuyafanyia tathmini mashirika mengi ya umma hasa makongwe yasiyo na tija yafutwe, kwa sababu yamedumu kwa hasara na kuwa mzigo kwa serikali.

Samia alisema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam baada ya kupokea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2021/22 ambayo imebaini kuwa kuna mashirika 14 ya umma yanayofanya kazi kwa hasara, sababu kubwa ikiwa kasoro za kiutendaji.

Alitoa mfano wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) kwamba limekuwa kongwe katika historia akiifananisha na makuzi yake na hadi sasa lipo lakini likiwa halina tija kwa taifa na kuhoji uhalali wa kuendelea kuwapo.

"Mashirika haya yafanyiwe tathmini kufikia hapa. Mengine hayajawahi kufanya kazi yakawa na matokeo chanya. Tangu niko sekondari nayasikia, sina kigugumizi cha kusema. NDC kwa mfano kwa wale wa umri wangu tangu tunatumia 'lifebuoy' (sabuni za kuogea) zinatoka nje na betri zetu National tunatengeneza hapa.

"Mpaka leo nipo kwenye kiti hiki kuna NDC. Ukitafuta ripoti lini walifanya vizuri labda awamu ya kwanza lilipoundwa. Kaangalieni haya mashirika yanakula tu pesa kutoka serikalini yenyewe hayaleti. Kila mwaka bajeti ya mashirika ipo hapo, wafanyakazi tunawalipa.

"Yale ambayo yanafaa yawepo lakini ambayo hayafai yafutwe. Yaliundwa yakafanye biashara, yanatumia gharama za serikali. Mashirika 300 na zaidi ya nini? Kama yapo yanayofaa yawepo na yasifutwe, si kwa faida yangu kwa faida ya nchi," alisema Rais Samia.

Rais Samia pia licha ya mashirika hayo, alisema ripoti hiyo imesema kuna mashirika ambayo yanafanya vizuri lakini mengi yanadorora.

"Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) limeshindwa kutoa huduma ya mawasiliano yaani simu. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), mwishowe utashindwa kutoa huduma. Bima ya afya ni tatizo kubwa.

"Biashara ya simu kwao imewashinda, wasimamie wenzao, washike mkongo wa taifa, wafanye mengine, wayasimamie kampuni za simu. Tutashindwa kutoa huduma kwa watu wetu, pamoja na kujenga vituo vya afya, kununua vifaa tiba vingi, tunaweza kushindwa kutoa huduma, licha ya kuwekeza," alisema Rais.

**MALIPO KUONGEZEKA**

Aidha, kuhusu malipo ya ankara ambayo huletwa kutokana na serikali kulipia miradi tofauti, alisema kuna tofauti ikilinganishwa na gharama zilizoko kwenye mikataba.

"Mfano kwenye ndege ya mizigo inayokuja, gharama ilikuwa dola milioni 37 lakini 'invoice' (ankara) ilipokuja ni dola milioni 86, hii imetoka wapi? Vifaa vimepanda bei, ulipopokea ulifanya nini? Wewe ulipopokea, wanaopokea invoice kwa raha zao, hawatufai.

"Angehoji, si kusema hii hapa 'invoice'. Vifaa vimeongezeka sababu ya UVIKO-19, 'over invoice' ziko nyingi sana. Mikataba hii ina tatizo sana. Tunaua nchi yetu wenyewe," alisema.

**MIFUKO HIFADHI**

Rais Samia alisema upande wa mifuko ya hifadhi ya jamii, nako kuna tatizo, kwa sababu mifuko iyo imekuwa ikiingia kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa tofauti na uwezo wao.

"Serikali lazima tuibebe, ili wafanyakazi wasikatwe haki zao," alisema Rais.

**TRA YATWISHWA ZIGO**

Rais alisema ili kuongeza mapato ya serikali Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeongezewa malengo zaidi lakini akasisitiza kuwa ili kufikia azma hiyo, lazima mifumo yake na ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), isomeke kiutendaji kwa pamoja.

Alisema ukusanyaji wa mapato ya serikali hususani kutoka TPA aliyoitaja kuwa ndilo lango kuu na upatikanaji fedha za umma ni duni kutokana na mifumo ya mamlaka hizo duni kutosomana kiutendaji.

"CAG amesema pia TRA na TPA hawasomani. Wakati bandari ndiko kunakokusanywa fedha na mifumo isiposomana vizuri maana yake watu wapate kuchomoa fedha, kuna tatizo gani la kufanya TRA na bandari msisomane.

"Tuwatake TRA na bandari mkae kitako mhakikishe mifumo inasomana. Nimeambiwa TRA kuna Wakorea wengi ambao wamekuja kwa sababu ya mifumo wasiondoke hadi isomane. Tatizo la bandari la siku nyingi na nimelisemea siku nyingi.

"Nimewaambia bandari mshirikiane na sekta binafsi kwa ajili ya uboreshaji mifumo pia 'transfer' (uhawilishaji) ya (wa) teknolojia. Fedha chungu nzima zinanunua vifaa vya bandari wakati sekta binafsi wanaweza kufanya kazi. Hakuna sekta binafsi ambayo itaweka fedha yake pale, akubali mifumo abakie hivyo, ataimarisha,"

# Samia: Waliotafuna fedha halmashauri wawajibishwe

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema fedha zinazotolewa kwa ajili ya maendeleo ya miradi mbalimbali katika mamlaka za serikali za mitaa (halmashauri) zimegeuka na kuwa kichaka, kwa kuwa ndiko chanzo cha upotevu wa fedha za serikali.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, Rais Samia ameagiza waliohusika katika upotevu huo wawajibishwe pamoja na kuzirejesha huku akitaka hatua zaidi zichukuliwe ili kumaliza tatizo hilo.

Rais Samia aliyasema hayo jana, Ikulu, jijini Dar es Salaam, wakati akipokea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2021/22. Ripoti hiyo imebaini kuwa katika halmashauri 180 nchini kumekuwa na upotevu wa mabilioni ya fedha zinazotolewa kwa ajili ya maendeleo pamoja na mikopo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

"Fedha za halmashauri mimi nasema huko ni pori, kwanza mifumo. Watu kama wameondoka kazini kwa ajili ya kustaafu, kutenguliwa, anaondoka na mashine ya POS (mashine kwa ajili ya ukusanyaji mapato ya serikali katika halmashauri). Ukiwauliza halmashauri wanasema mashine ameondoka nayo fulani.

"Ulaji wa pesa mbichi ni mkubwa sana kwenye halmashauri, mheshimiwa waziri, ulaji wa pesa mbichi halmashauri uondoke. Matumizi ya EFD (mashine za kielektroniki za ukusanyaji mapato) halmashauri wanajihisi hawahusiki kabisa na matumizi ya EFD kwenye maeneo yao. Kuna taarifa hata taasisi za serikali zikinunua haziombi risiti. Sasa sisi serikali tutamwambia nini mtu binafsi kama sisi hatufanyi? Haiwezekani, tubadilike sana," alisema Rais.

Alisema pia ripoti ya CAG inaonyesha ulaji wa fedha za UVIKO-19, akisema anatarajia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) itakuja na majibu na kwamba fedha hizo zilipwe.

"TAKUKURU watakuja na majibu. Aidha (ama) fedha wazilipe au wawajibike. Kama umechukua leo, utalipa keshokutwa, lazima walipe," alisisitiza.

Rais Samia aliipongeza TAKUKURU kwa kufanya vizuri na kuokoa fedha, baada ya kuingilia mikataba na kwamba taasisi hiyo kutokana na kazi yake imefikia asilimia 60 ya uchunguzi na matokeo ya mahakamani, akisema awali haikufikia hata asilimia 40.

"Tumesikia CAG akisema kuna mikataba ya ovyo, tunaingia tu na huko ndiko kwenye upotevu wa fedha," alisema Rais Samia.

Alisema ucheleweshaji wa manunuzi vifaa vya serikali kupitia kampuni binafsi iliyoingia mkataba na serikali, bado kuna uchelewaji na kwamba uwepo mfumo mwingine wa kufanya shughuli ya ununuzi ili kuongeza tija.

**WAWAJIBISHWE**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema anashangazwa na watumishi wa umma wanaohusika na matumizi mabaya na upotevu wa fedha, kutochukuliwa hatua za kinidhamu wala kisheria na kuutaka utumishi, kuchukua hatua.

"Nizungumze na Utumishi (Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), hawa watu ambao fedha zinakuwa na matumizi hovyo, usimamizi ni mdogo tunawaangalia tu. Ripoti ya mwaka jana, mwaka juzi na mwaka huu, ofisi mtu ni yule yule, yuko pale pale pamoja na upotevu wote huu.

"Kama hamuwezi kuwatoa basi angalau wabadilisheni. Wapelekeni ambako hakuna fedha nyingi, ili wakaonje joto ya jiwe, hatuwezi kupokea ripoti tatu, mtu yuleyule yuko palepale," alisema Rais Samia.

Alisema pamoja na hayo kuhusu changamoto kubwa kwenye Utumishi ikiwamo ya vitendea kazi, serikali itafanyia kazi kulingana na bajeti inavyoruhusu.



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza baada ya kupokea taarifa ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2021/2022, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Mikopo bil. 88/- halmashauri 'yayeyuka'

**Na Maulid Mmbaga**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amebaini kuwa mamlaka 180 za serikali za mitaa zimeshindwa kukusanya mikopo iliyotolewa kwenye vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu yenye jumla ya Sh. bilioni 88.42.

Akiwasilisha Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/22, jana jijini Dar es Salaam, CAG alisema hali hiyo imetokana na kutokuwa na ujuzi wa kutosha kwenye idara ya maendeleo ya jamii.

Alisema idara hizo katika ngazi ya mamlaka za serikali ya mitaa hazikuwa na ujuzi wa kutosha wakati wa kufanya upembuzi yakinifu kwa vikundi vilivyoomba mikopo, kuvisimamia katika kufanya urejeshaji wa mikopo na kutoa mafunzo ya biashara kwa wanufaika.

"Kati ya kiasi hicho, Sh. bilioni 2.25 zinahusiana na vikundi vilivyoacha shughuli za biashara na kuleta mashaka juu ya urejeshwaji wa mikopo hiyo. Pia nilibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa ziliitoa Sh. milioni 895.94 kwa vikundi 48 ambavyo havikuwapo," alisema Kichere.

Kutokana na ukubwa wa mfuko huo na manufaa yake, alipendekeza serikali kuboresha usimamizi na kuangalia uwezekano wa kushirikisha taasisi za kifedha za serikali zenye ujuzi wa kufanya shughuli hizo ili kuboresha ufanisi wake na kuongeza tija.

Kutokana na taarifa hiyo, Rais Samia baada ya kupokea ripoti hiyo, alisema mfumo unaotumika wa utoaji wa mikopo hiyo kupitia halmashauri hautawafikisha popote huku akipendekeza kutumika mfumo mbadala wa kibenki.

"Fedha ikusanywe kila halmashauri ipigiwe hesabu yake kwa mwaka huo asilimia 10 yake ni kiasi kadhaa ipelekwe benki, tutakayokubaliana baada ya kubadilisha mfumo ili vijana, wanawake na wenye ulemavu wakachukue pesa benki kwa sababu huko ukitaka utarudisha, hutaki utarudisha," alisema.

Aidha, katika usimamizi wa ununuzi katika mamlaka za serikali za mitaa, CAG Kichere alibaini kwamba mamlaka 16 zililipa Sh. bilioni 1.8 kwa kazi za ujenzi bila nyaraka za vipimo kuthibitisha kazi zilizofanyika.

Hata hivyo, CAG Kichere alisema mamlaka 98 za serikali za mitaa hazikuwasilisha Sh. bilioni 11 zilizokusanywa katika akaunti husika za benki na kwamba hiyo inatokana na ufuatiliaji duni na kutofanyika kwa suluhisho la hesabu mara kwa mara. Pia alisema mawakala wa ukusanyaji mapato katika mamlaka 10 za mitaa haukuwasilisha Sh. bilioni 4.12 kwenye benki, huku akiwashauri wakurugenzi wa mamlaka husika kuhakikisha fedha zote ambazo hazikuwasilishwa zinawasilishwa na kuwekwa benki kwa mujibu wa sheria na taratibu.

**UPUNGUFU ULIPAJI KODI**

Katika hatua nyingine CAG alisema amebaini upungufu katika ukusanyaji wa mapato ndani ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Alisema taarifa ya TRA ambayo waliifanyia kazi na kuihakiki ilionyesha kuwa Tanzania Bara, ilikusanya jumla ya Sh. trilioni 20.94 ambazo ni chini ya makadirio ya Sh. trilioni 21.78 yaliyowekwa, hivyo kuwa na upungufu wa malengo kwa Sh. bilioni 833 sawa na asilimia 3.8.

Mbali na TRA amesema taasisi kadhaa pia zimebainika kukusanya mapato nje ya mfumo wa kielektroniki wa malipo serikalini (GePG), hivyo kuibua shaka kama mapato yote yanaingia serikalini.

Kichere alisema miongoni mwa taasisi hizo ni Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ambayo ilikusanya takribani Sh. bilioni 68.24 nje ya mfumo.

Kichere alizitaja taasisi zingine kuwa ni Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Sh. bilioni 151.54) na Shirika la Magereza (Sh. milioni 900.69) zote ikiwa zimekusanywa nje ya mfumo wa GePG, hivyo kukiuka maelekezo ya serikali ambayo yanasema fedha zote zikusanywe ndani ya mfumo huo.

Pia alisema kuna udhaifu katika ukusanyaji wa kodi za nyumba kwa taasisi za serikali kwa miezi 10 hadi 103, hatua ambayo imesababisha kupotea kwa takribani Sh. bilioni 13.

Kadhalika, alisema ukaguzi umebaini taasisi 21 kushindwa kuwasilisha kodi ya zuio ya Sh. milioni 749 kwa TRA na zingine 15 hazikukata kodi ya Sh. milioni 713.70 na sita zilizuia kodi lakini hazikuwasilisha TRA kiasi cha Sh. milioni 35.

Kwa mujibu wa ripoti ya CAG, baadhi ya taasisi hizo ni Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ambayo haikukatwa kodi ya Sh. milioni 442, Kampuni ya JKT (Sh. milioni 162), RUWASA (Sh. milioni 56 na Wakala wa Huduma za Ununuzi wa Umma (Sh. milioni 34).

Alisema taasisi zilizokata lakini hazikuwasilisha kodi ya zuio kwa TRA ni Wizara ya Viwanda na Biashara (Sh. milioni 16) na Chama cha ACT-Wazalendo milioni 8.5.

"Serikali inapoteza mapato kutokana na kutokatwa kwa kodi ya zuio na kushindwa kuwasilisha kodi hiyo kwa TRA, hivyo kuathiri shughuli za serikali zilizopangwa. Maofisa masuhuli wahakikishe kodi hiyo inakatwa na kupelekwa TRA kama sheria inavyoelekeza," alisema.



Katibu wa Ngome ya Vijana Taifa wa Chama cha ACT- Wazalendo, Mwanaisha Mndeme, akizungumza wakati wa mkutano wa kutoa tamko la pamoja la kupinga ndoa za utotoni uliojumuisha mashirika 58 ya haki za wasichana Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# SAUT kurejesha shahada za madaktari 162

**Na Vitus Audax,** MWANZA

CHUO Kikuu cha Mtakatifu Agustino Tanzania (SAUT) kimesema kiko tayari kurejesha uhalali wa shahada za madaktari 162 waliofutiwa shahada zao hivi karibuni. Kauli hiyo imetolewa jana na Mwenyekiti wa Seneti ya vyuo vya SAUT nchini, Balozi Profesa Costa Ricky Mahalu, ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo hicho Kampasi ya Mwanza wakati akitoa ufafanuzi wa taarifa za chuo hicho kuwafutia matokeo madaktari hao 162.

Alifafanua kuhusu kufukuzwa kazi kwa wafanyakazi wa utawala wawili katika Chuo Kikuu Kishiriki cha SAUT kinachojulikana kama Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Mt. Fransisco (SFUCHAS) kwa kushiriki kutoa nakala za matokeo kwa madaktari hao baada ya mfumo wa matokeo kubadilishwa kinyume cha sheria.

Balozi Mahalu alisema mwaka 2020 katika chuo cha SFUCHAS uongozi wa chuo hicho bila kuifahamisha Seneti ya vyuo vya SAUT yenye mamlaka kisheria ya kuidhinisha matokeo pamoja na shahada zote, waliamua kukaa na kuchukua mfumo mwingine wa masahihisho ya matokeo ya mitihani na kutengeneza nakala za matokeo nyingine kupitia mfumo mpya wa matokeo uliobadilishwa na kuwapatia wanafunzi 389 waliohitimu mwaka 2015 mpaka 2019.

Aidha, alisema kati ya wahitimu 389 ni 216 ndio waliorudisha nakala hizo baada ya chuo hicho kutangaza mwaka 2021 zirudishwe ili waendelee kutumia zenye matokeo ya awali.

Alisema, madaktari 11 walirudisha wakati seneti inakaa ili kubatilisha matokeo yao na baada ya kubatilisha madaktari 15 walirudisha huku wakisalia 147 wakati wote walitakiwa kurudisha nakala hizo ili seneti hiyo ikikaa tena iidhinishe matokeo ya awali na kuruhusiwa kuendelea na kazi zao.

"Hii ni kwa mujibu wa Sheria za Tume ya Vyuo Vikuu Tanzani (TCU) na wote waliobatilishiwa shahada hizo hawatoruhusiwa kuendelea na shughuli zao za kitaaluma ikiwa ni pamoja na kuhudumia wagonjwa katika vituo pamoja na hospitali yoyote ndani na nje ya nchi," alisema Balozi Profesa Mahalu.

Alisema wakirejesha nakala hizo wote seneti hiyo itakaa tena na kujadiliana na kuhalalisha tena kupitia za awali za matokeo ili waweze kuendelea na shughuli zao.

"Tatizo katika nakala hizi ni kwamba unakuta matokeo ya mwaka 2015-2019 alama C ilikuwa ni maksi 50 huku katika mfumo mpya ambao walibadilishiwa nakala hizo maksi 50 ilikuwa alama B na walibadilishiwa bila kuifahamisha seneti yenye mamlaka ya kuidhinisha nakala hizo," alisema.

Vilevile, alisema wahitimu hao walifutiwa matokeo yao kupitia Sheria ya Vyuo Vikuu nchini ya mwaka 2005 Ibara ya 45 inayoipa mamlaka seneti kubatilisha matokeo ya wahitimu hao na kikao pekee cha seneti hiyo ndicho kinachoweza kuhalalisha matokeo na shahada zao.

Katika hatua nyingine Balozi Mahalu alisema seneti hiyo ina uwezo wa kubatilisha matokeo pamoja na shahada za wahitimu wao endapo watakiuka maadili ya kazi zao pamoja na kujihusisha na ubadhirifu wa aina yoyote katika jamii.

Aidha, alitahadharisha wahitimu wote kuwa makini na shahada walizotunukiwa kwa kuwa sio mali zao bali ni za vyuo vikuu husika na seneti za vyuo hivyo ndizo zenye mamlaka ya kuzi idhinisha na kuzibatilisha.

# Mwinyi: Asitokee kiongozi kuwatisha watoa taarifa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka viongozi wa umma kuwajibika kwa kero na changamoto wanazowasilishiwa na mfumo wa Sema Na Rais (SNR).

Alisema wapo baadhi ya viongozi wasiotaka kutatua changamoto hizo kwa kuwa hawaoni umuhimu wake na kuonya atawachukulia hatua.

Kadhalika alibainisha kupitia mfumo huo kuna utambuzi wa kitakwimu kujua kiongozi au taasisi zisizofanya vizuri na sasa wakati umefika kila mmoja aone umuhimu wa kuwajibika.

Alisema hayo jana kwenye kikao kazi cha maadhimisho ya miaka miwili tangu kitengo cha Sema na Rais Mwinyi (SNR) kilipoasisiwa. Kitengo hicho kipo chini ya Ofisi ya Rais Ikulu.

Akizungumzia mafanikio ya mfumo wa SNR kwa kipindi hicho cha miaka miwili, alisema umeleta tija kwa wananchi ambao changamoto zao zimetatuliwa kwa kiasi kikubwa na ataendelea kuusimamia vyema.

Alizungumzia suala la taarifa za ubadhirifu wa mali za umma na kuonya asitokee kiongozi yeyote kuwatisha wanaowasilisha kero au changamoto kupitia mfumo wa SNR na kuahidi hatua zitachukuliwa dhidi ya kiongozi huyo.

Aliahidi mtoa taarifa atalindwa na kuwaambia maofisa wa SNR wafanye kazi zao bila woga.

Vilevile, Dk. Mwinyi alisema anathamini uhuru wa Mahakama na Serikali itayafikisha mbele ya haki matatizo yatakayopelekwa na SNR mahakamani kwa Jaji Mkuu ayashughulikie na kuondoa kasoro zinazojitokeza.

Katika msingi wa utawala bora, Rais Mwinyi alibainisha kuwa serikali haina haki kuingilia mhimili wa Mahakama, lakini ina wajibu kuwasilisha changamoto wazishughulikie.

Aliwataka Makatibu Wakuu na Wakuu wa Taasisi za Serikali kuwajibika moja kwa moja na kuhakikisha mfumo wa SNR unafanya kazi vizuri na kwa wakati kutatua changamoto za Wazanzibari.

Aidha, aliipongeza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Wizara ya Habari Vijana Utamaduni na Michezo na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa juhudi zao za kutatua changamoto kupitia mfumo huo.


## BONITE BOTTLERS LIMITED

### Advertisements of Employment

1. **Mechanical Technician**
   **Qualification:**
   - Applicant should be a holder of VETA level III in Mechanical Engineering from a recognised Institution.

   **Key skills & Abilities:**
   - Ability to maintain and troubleshooting all the mechanical equipment to acceptable and approved standards for efficient operation and to ensure smooth running of the line and service equipment by close communication with other staff.
   - Ability to operate machines as directed and to ensure they are running smoothly, efficiently and kept clean as required.
   - Able to work independently with minimum supervision
   - Self motivated, flexible person and a good team player.
   - Compliance to safety requirement at work place

2. **Electrical Technician**
   **Qualification:**
   - Applicant should be a holder of VETA level III in Electrical Engineering from a recognised Institution.

**Key skills & Abilities:**
- Ability to maintain all the electrical equipment to acceptable and approved standards for efficient operation, and to ensure the smooth running of the line and service equipment by close communication with other staff.
- Ability to operate the machines as directed and to ensure they are running smoothly and efficiently as required and kept clean as required.
- Ability to ensure the correct electrical functioning of electrically operated equipments on the premises.
- Able to work independently with minimum supervision
- Self motivated, flexible person and a good team player.
- Compliance to safety requirement at work place

√ **Experience:** Six months and above in Mechanical/Electrical field
√ **Location:** Moshi.

**Mode of Application:**
All applications accompanied with cover letter, photocopies of certificates and CVs to be sent to the undersigned, to reach him not later than 11/04/2023.

**The Managing Director,**
**Bonite Bottlers Ltd,**
**P. O. Box 1352,**
**MOSHI.**

217346202

## HABARI KITAIFA

# Upelelezi kesi ya Sabaya wakamilika

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BAADA ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, mkoani Kilimanjaro kusota kwa siku 302 rumande kwa kesi namba 2 ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha, upande wa Jamhuri umesema upelelezi umekamilika na kuomba tarehe ya karibu kwa ajili ya kukabidhi vibali.

Mbele ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, Mwendesha Mashtaka, Sabitina Mcharo, alidai upelelezi umekamilika na kuomba mahakama kuwapa tarehe ya karibu kwa ajili ya kuweka vibali pamoja na kuendelea na taratibu nyingine kwa mujibu wa sheria.

"Mheshimiwa upelelezi umekamilika na tunaomba tarehe ya karibu kwa ajili ya kuwasilisha nyaraka pamoja na kusikiliza maelezo ya awali," alidai Sabitina.

Upande wa utetezi uliongozwa na mawakili Hellen Mahuna pamoja na wakili Mosses Mahuna. Kukamilika kwa upelelezi kutasaidia mteja wao kutambua alipo ikiwa tayari amekaa gerezani zaidi ya siku 302.

"Mheshimiwa kwa upande wa mshtakiwa tumefurahi kusikia upelelezi umekamilika na tunaomba utupatie ahirisho fupi ili tuweze kuja tarehe za karibu ili tuweze kuendelea na shauri hilo," alidai Mahuna na kuongeza kuwa "tunategemea kuanza kusikilizwa kwa haraka ili kumsaidia mteja wetu kupata haki na kujua hatima yake."

Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, Salome Mshasha, aliaihirisha kesi hiyo hadi Aprili 5, mwaka huu.

Sabaya, mara ya mwisho kufikishwa mahakama hapo ilikuwa ni Desemba 5, mwaka jana baada ya kesi hiyo kuahirishwa kutokana na hakimu mwenye mamlaka kuwa na majukumu mengine.

# USAID yazindua programu ya kuwajengea uwezo vijana

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) limezindua programu ya mafunzo ya kujitolea kwa vitendo na ushirika kwa lengo la kujengea uwezo vijana wataalamu katika nyanja ya mabadiliko ya kijamii na ya kitabia kwa afya.

Hii ni sehemu ya mpango wa kuimarisha uwezo wa mradi wa USAID wa 'Breakthrough ACTION' nchini Tanzania ambao ni mradi wa Mabadiliko ya Tabia ya Kijamii (SBC) ulioundwa ili kutoa msaada wa kiufundi kwa serikali ya Tanzania ili kuboresha sera na mfumo wa utekelezaji kuhusu shughuli za mradi wa Mabadiliko ya Tabia ya Kijamii.

Lengo la mradi ni kuchochea fursa kwa watanzania kuboresha hali zao za afya kwa kubadilisha kanuni za kijamii na kitamaduni na kuunga mkono matumizi ya mbinu bora za kiafya.

Programu hiyo iliyozinduliwa hivi karibuni, iliweka bayana malengo na madhumuni ya programu, mashirika yanayohusika, na umuhimu na manufaa ya programu hii katika kuleta matokeo chanya ya maendeleo ya sekta ya afya, na pia kutoa ushuhuda kutoka kwa washiriki wa awali wa programu. Hafla hiyo ya uzinduzi ilihudhuriwa na wakilishi kutoka Wizara ya Afya, USAID na mashirika mengine na zikieleza dhamira yao ya kukuza elimu, maendeleo ya kitaalamu na maendeleo ya kijamii.

"Tunashukuru kwa msaada ambao USAID umetoa kwa Wizara yetu katika kujenga uwezo ili kuleta mabadiliko ya kijamii na tabia kwa Sekta ya afya," alisema Simon Nzilibili ambaye ni Ofisa Programu Sehemu ya Elima ya Afya kwa Umma kutoka Wizara ya Afya.

"Tunapenda kuishukuru USAID kwa kuibua programu hii ya mafunzo ya kujitolea kwa vitendo na ushirika na tunatarajia kuendeleza ushirikiano ili kwa pamoja tutatue changamoto za afya nchini Tanzania," aliongeza.

Dk. Ify Udo, Meneja Afya ya Jamii kutoka USAID alisema: "Programu ya mafunzo ya kujitolea na ushirika ni moja ya hatua katika kuwajengea uwezo kizazi kijacho cha wataalamu wa mabadiliko ya kijamii na tabia. Kupitia uzoefu wa vitendo na fursa mchanganyiko za kujifunza, vijana wataalamu watapata ujuzi na maarifa wanayohitaji ili kuendeleza ubunifu, mwenendo mzuri na maendeleo endelevu katika Sekta ya Afya."

Aliongeza kuwa: "Tuna furaha kushirikiana na Wizara ya Afya na mashirika mbalimbali katika kutekeleza programu hii na tunatarajia matokeo chanya katika maendeleo ya afya."

Programu hiyo imeundwa kutoa fursa kwa vijana wataalamu kutumia nadharia na uzoefu wa vitendo wa mabadiliko ya tabia na kijamii katika mazingira halisi. Programu hii inatumia mbinu mbalimbali za kujifunza zikiwemo mafunzo ya darasani, mafunzo kazini, na ushauri ili kuhakikisha washiriki wanapata uzoefu wa kina na wanajifunza kwa vitendo.

Halfa ya uzinduzi ilitoa fursa ya kuonyesha athari chanya za programu na kuleta hamasa kwa wataalamu wa baadaye ili kuwapa msukumo wa uvumbuzi na maendeleo katika nyanja ya mabadiliko ya kijamii na kitabia. USAID inawahimizwa washiriki wote katika sekta ya afya kuunda fursa za mafunzo ya kujitolea kwa vitendo na kuwekeza katika maendeleo ya kitaaluma ya vijana wataalamu.


## FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED
## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

1st Housing

**Imetolewa chini ya kanuni ya 58 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Mikopo ya Nyumba) ya Mwaka 2015.**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2022

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Mwaka wa sasa 31st Dec. 2022 | Mwaka uliopita 31st Dec. 2021 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,532 | 615 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 3,601,363 | 3,601,639 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 6,695,407 | 945,171 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 19,561,504 | 13,570,278 |
| 12 | Mali Nyingine | 706,753 | 575,929 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,622,000 | 1,622,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 323,876 | 449,612 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **32,512,435** | **20,765,244** |
| | | | |
| B. | B. DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 911,787 | 488,087 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,054,642 | 1,008,249 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 41,070 | 41,070 |
| 27 | Dhima Nyingine | - | - |
| 28 | Madeni | 12,003,729 | 1,010,685 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **14,011,228** | **2,548,091** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **18,501,207** | **18,217,153** |
| | | | |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,800,000 | 21,800,000 |
| 32 | Malipo juu ya bei ya hisa | - | - |
| 33 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | (3,678,678) | (3,911,640) |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 284,054 | 232,962 |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 95,831 | 95,831 |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 38 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **18,501,207** | **18,217,153** |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 40 | Mikopo Chechefu | 561,178 | 329,009 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 135,812 | 55,648 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 56.91% | 87.73% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2.85% | 2.39% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 2160.30% | 2825.75% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 60.17% | 65.35% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 91.84% | 88.34% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 86.81% | 18.16% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 56.57% | 2.94% |

Taarifa hapo juu inatokana na taarifa ya fedha ya mwaka ulioishia Disemba 31, 2022 ambayo imendaaliwa kutokana na viwango vya kimataifa vya uaandaji wa taarifa za fedha (IFRS). Taarifa hii ya fedha imekaguliwa na mkakuguzi aliyethibitishwa, Ernst & Young - Certified Public Accountants na kupata hati safi.

| Jina na Cheo : | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Sasa M. Chonza **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | (Imesainiwa) | 30.03.2023 |
| Amulike E. Kamwela **(Ofisa Mkuu wa Fedha)** | (Imesainiwa) | 30.03.2023 |
| Isambo Binde **(Meneja - Mkaguzi wa Ndani)** | (Imesainiwa) | 30.03.2023 |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2022

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| S/No | Maelezo | Mwaka wa sasa 31st Dec. 2022 | Mwaka Uliopita 31st Dec. 2021 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,855,309 | 2,487,835 |
| 2 | Gharama za Riba | (1,000,506) | (122,779) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **2,854,803** | **2,365,056** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (96,711) | (17,041) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **167,890** | **130,606** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (1,480) | (1,464) |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 93,770 | 53,781 |
| | 6.3 Gawio | 27,590 | 35,130 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 48,010 | 43,159 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(2,619,191)** | **(2,229,229)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,568,574) | (1,165,923) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1,050,617) | (1,063,306) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **306,791** | **249,392** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (22,737) | (16,430) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **284,054** | **232,962** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **284,054** | **232,962** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 23 | 19 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 1.30 | 1.07 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 |
| | | | |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.07% | 1.12% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.55% | 1.28% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 86.65% | 89.32% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 11.84% | 12.89% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2022

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

(Kiasi kwa shilingi elfu)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa (2022)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **21,800,000** | **-** | **(3,703,026)** | **24,348** | **-** | **95,831** | **18,217,153** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 284,054 | - | - | - | **284,054** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (37,980) | 37,980 | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **21,800,000** | **-** | **(3,456,952)** | **62,328** | **-** | **95,831** | **18,501,207** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka uliopita (2021)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **21,800,000** | **-** | **(3,911,640)** | **-** | **-** | **95,831** | **17,984,191** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 232,962 | - | - | - | **232,962** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | (24,348) | 24,348 | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **21,800,000** | **-** | **(3,703,026)** | **24,348** | **-** | **95,831** | **18,217,153** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi).

| Jina: | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **Conrad D'souza** Mwenyekiti | (Imesainiwa) | 30.03.2023 |
| **Vinod Rustagi** Mkurugenzi | (Imesainiwa) | 30.03.2023 |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2022

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| S/No | | Mwaka wa sasa 31st Dec. 2022 | Mwaka Uliopita 31st Dec. 2021 |
|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **306,791** | **249,392** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 297,712 | 321,866 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (6,075,097) | (7,376,039) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 423,700 | 75,000 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 119,974 | (50,276) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (172,837) | (44,042) |
| | - Kodi iliyolipwa | (19,978) | (12,917) |
| | - Mengineyo | (4,195) | (5,640) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(5,123,930)** | **(6,842,656)** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | 27,590 | 35,130 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (30,904) | (48,243) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 276 | (1,059,492) |
| | Mengineyo (bainisha) | (2,348) | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(5,386)** | **(1,072,605)** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Ulipaji wa deni la Lease Liability | (99,297) | (95,154) |
| | Mengineyo (Mkopo kutoka TMRC) | 10,993,044 | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **10,893,747** | **(95,154)** |
| | | | |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na** | **5,764,431** | **(8,010,415)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka | 945,786 | 8,921,409 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo ya mabenki | (13,278) | 34,792 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka** | **6,696,939** | **945,786** |




17347202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Ujio Kamala Harris mwanzo ushirika mpya

**MAKAMU** wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, karibu Tanzania. Ndivyo leo tunavyoamka na kumkaribisha mgeni wa taifa letu ambaye ameanza ziara ya kiserikali akitokea Ghana.

Tunapompokea Makamu wa Rais wa Marekani, tunakubali kuwa Afrika ikiwamo Tanzania inahitaji washirika madhubuti kuzitambua na kuzikabili changamoto na matatizo makubwa yanayoikumba dunia na yanayoongezeka kila siku, lakini yakiumiza zaidi Afrika.

Tukiangalia tuna changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, joto zaidi, vipo vimbunga vikubwa baharini, ukame, upepo mkali unaokausha maji na mimea na njaa, yote yakiathiri mataifa yenye uchumi unaoendelea kama ya kwetu.

Pamoja na hayo kuna magonjwa ya milipuko yanayoua kwa kasi kama COVID-19, Ebola na Marburg ambayo imeripotiwa Bukoba hivi karibuni yote hayo yakitishia maisha na hatima ya uchumi na uwekezaji wa taifa hili la Afrika. Kwa upande mwingine mapinduzi ya teknolojia duniani kuanzia kwenye matibabu, kilimo, TEHAMA, nishati -umeme wa maji, upepo, jua na vyanzo vingine, yanahitajika pia kuinufaisha Afrika.

Yote yanaalika ushirikiano wa kweli kuyatatua kuanzia kufunza wataalamu, kuchangia vifaa, fedha na mbinu za kukabiliana nayo lakini kwa utaratibu unaoleta kunufaika au 'win -win' game', badala ya upande mmoja kuumia zaidi huku mwingine ukineemeka.

Kama wadau wa habari na mawasiliano tunautazamia mkakati mpya wa Marekani unaokuja na Kamala Harris, kusaidia Afrika iwe bora kwa kuwa ndilo bara linaloweza kuzalisha kila kitu na lenye kile kinachohitajika duniani iwapo litakuwa na maendeleo badala ya kuwa jumba la maskini kama ilivyo sasa ndiyo maana tunasisitiza kuwe na juhudi za pamoja.

Ujio wa Makamu wa Rais uihakikishie Afrika jinsi Marekani inavyolenga kuleta nuru mpya kiuchumi, kisiasa, kiteknolojia, tiba na kidemokrasia ili kila upande unufaike na kuweka mazingira bora ya kiuwekezaji, kuinua uchumi, jamii na pia kusaidia kukabiliana na vitu hatarishi kama taka za kielektroniki na plastiki zisiendelee kuathiri watu na mazingira.

Ni ukweli kwamba China na Urusi zinachipukia na kutaka kushirikiana na kuungwa mkono na Afrika, lakini, cha msingi ni Waafrika kujitambua kuwa hawahitaji kupangiwa marafiki au maadui bali, ishirikiane kila mmoja awe China, India au Falme za Kiarabu kujenga ushawishi na ushirikiano wenye matokeo bora kwa faida ya kila upande.


Ni wazi kuwa Marekani ni mshirika wa Afrika mwenye sehemu yake kwa sababu za kihistoria na kiuchumi ambazo Waafrika wanazifahamu, hivyo ni vyema ushirika huo ukawa wa tija na manufaa zaidi kuliko hapo awali ili kujiongezea ushawishi.

Kwa Afrika, Amerika ni mshirika wa kipekee, ndiyo maana sasa katika kuanzisha harakati mpya, taifa hilo kubwa kisiasa, kiuchumi, kijeshi, kiteknolojia na ubunifu linatarajiwa katika ziara ya Harris, lichangie kusaidia kupata amani ya kudumu DRC.

Umoja wa Mataifa (UN) umekuwapo DRC, Umoja wa Afrika upo lakini pia hata majeshi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni wadau wa kufikia amani ya DRC, ni ombi la Afrika sasa Marekani isaidie kupata ufumbuzi wa kupatikana haki na kumaliza mgogoro wa taifa hilo unaoshuhudia vifo vya maelfu ya watu na kuinyong'onyeza Afrika. Kwa vile Marekani inaifahamu na imetanzua migogoro mikali kadhaa hakuna shaka Afrika itaona ufanisi wake katika kufikia juhudi za kurejesha na kulinda amani ya DRC na hasa sasa inapoanzisha ushirikiano mpya, anaouhubiri Harris.

Tunawashauri viongozi wa Afrika wasitazamie mambo bila kutoa ya kwao ya moyoni waiambie Amerika yale wanayoyatazamia na namna bora ya kuyafanikisha kwa kuangalia vipaumbele vyao kwenye ushirika huo ili uwe na tija.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanaoziba njia za maji mvua, wajue wanaibua madhara kwa mazingira

Na Yasmine Protace

**KWETU** jamaa wazaliwa wa vijijini na maeneo ambayo yana milima na mabonde, pia penye ukame tunaifahamu vyema mvua ni nini kwa binadamu, kuliko tafsiri iliyoko ya kawaida.

Hiyo ni bidhaa inayogusa moja kwa moja maisha ya binadamu mahali aliko, iwe uzalishaji chakula, kupata maji ya matumizi ya kila siku majumbani na afya ya binadamu, wanyama na mimea ambayo ni sehemu ya uzalishaji shambani. Kwa kifupi tumeshaambiwa 'maji ni uhai.' Sasa ni msimu wa mvua, ingawaje inapishana kati ya sehemu moja na nyingine. Tumefahamishwa na mamlaka husika, hali kadhalika tunashuhudia kila mahali nchini hali ya mvua, ingawaje kuna maeneo nchini tunaambiwa kutakuwapo shida ya mvua.

Ikinyesha kwa wastani na wakati unaotakiwa, huwa ni mazingira ya neema ikikidhi mahitajio ya matumizi mbalimbali; shambani, maji ya kunywa, hata hali ya hewa inakuwa safi.

Penye kinyume chake nacho kinakaribisha msamiati 'kizuri hakikosi kasoro'. Iwe mvua ya ziada au punguful, watumiaji binadamu, mimea na mazingira wanaangukia magumu. Hata hivyo, inabaki kwa ujumla, mvua ni neema kwa namna moja au nyingine, kila pale inaponyesha.

Mvua ina namna yake ya kunyesha. Huwafikia watu na mazingira yao katika mfumo asilia na watu wanapoziba njia zake mvua, huishia hatua ya kuwasababishia wakazi jirani majanga ya kufurika maji na nyufa katika makazi yao.

Niuase umma tunaoishi nao kwamba, katika maeneo tuliyopo, pindi mvua zinaponyesha, maji yake huelekea kila mahali na ndio maana, baadhi ya watu huyaelekeza katika maeneo mengine ili yasiwaletee madhara katika miji ya watu.

Lakini cha kushangaza, ni baadhi ya watu pamoja na mvua kunyesha maji yanapita katika maeneo yao na kuingia barabarani,wamekuwa wakiziba njia za mvua, ili maji yasipite na yajae katika majumba ya watu.

Kwa kufanya hivyo, wanakosea nyumba zinajaa maji na kuweka nyufa, pale njia zake zinapozibwa zinalazimisha kutunga mapito mapya na ndio unakuwa mwanzo wa shida hizo.

Maji ya mvua hayazuiliki hata siku moja na kinachotakiwa ni kuyaacha yapite katika njia zake na yaelekee yanapokwenda na sio kuyazuia.

Kwa yeyote anayeendelea kuyazuia, maana yake anasababishia watu kupata maradhi, kutokana na maji kujaa katika nyumba, hata kusababisha majumba kubomoka kwa kuingiliwa na maji.

Hivyo, watu mnaoziba njia za maji, muangalie na madhara ambayo yatawakuta wale ambao mnawazibia njia za maji ya mvua kupita.

Ndio maana hata ukiangalia kila penye ujenzi, huwa wanaelekeza maji pa kupita na kama yasipopata mwelekeo, ndio unakuwa mwanzo wa changamoto iwe penye ujenzi wa nyumba au barabara, panajaa maji.

Inasisitizwa kiufundi na kimazingira, kama watu wameweka njia za kuelekeza maji ya mvua, tunajinusuru na swali la wana mazingira "inakuwaje njia ya maji izibwe, hata kuangusha nyumba za watu?"

Siku zote ni vyema ubinadamu na busara ukawepo katika kukabaliana na maji kwa manufaa yetu, wenzetu na mazingira yanayotuzunguka.

Walau nashukuru kwamba kuna maendeleo sasa, mara zote kuna mwamko wa kimazingira unaochukua nafasi katika ujenzi wa namna mbalimbali.

Mojawapo inatajwa ni kupitia mamlaka za kiserikali, katika halmashauri mbalimbali nchini, ikizingatiwa kipengele cha haki na usawa na mazingira ya umma katika shughuli za ujenzi katika sehemu mbalimbali nchini, kulingana na matakwa na mahitaji ya mahali hapo.

Hiyo imekuwa na manufaa makubwa kutetea kanuni za mazingira nchini, hata kupunguza matukio ya maji kuchepushwa mkondo wake, au usahihi wa mahali stahiki kwa kufanyika ujenzi na mambo yanayofanana nayo.

# Mbaazi Tanzania zapata soko India

Na Joseph Mwendapole

SERIKALI imesema imepata soko la uhakika la tani 200,000 za mbaazi katika masoko ya India.

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alisema hayo juzi wakati akizungumza na Balozi wa India nchini, Binaya Srikanta Pradhan.

Dk. Kijaji alikutana na balozi huyo kuzungumzia namna ya kuendeleza uhusiano wa kibiashara na uwekezaji baina ya Tanzania na India.

Waziri Kijaji alisema serikali imeweka mazingira mazuri kwa wawekezaji, hivyo aliwakaribisha wawekezaji wa India kuwekeza nchini katika sekta mbalimbali hususani viwanda vya kutengeneza dawa na vifaa tiba.

Alisema kuna maeneo mengine mazuri ya kuwekeza kama uchumi wa bluu na viwanda vya kuongeza thamani mazao ya kilimo kama parachichi na mbaazi zinazohitajika kwa wingi katika soko la India.

Katika mazungumzo hayo, Dk. Kijaji alimhakikishia balozi huyo kuwa Tanzania iko tayari kupokea wawekezaji wenye nia ya kuwekeza katika sekta ya anga, utalii, kilimo na afya hususan katika viwanda vya dawa na vifaa tiba ili kupunguza gharama za uagizaji bidhaa hizo nje ya nchi.

Aidha, alimshukuru balozi huyo kwa upatikanaji wa soko la uhakika la mbaazi za Tanzania nchini India na kushauri wawekezaji kutoka nchini humo kuja kuwekeza katika viwanda vya kuongeza thamani katika mazao ya kilimo.

Waziri aliwahamasisha wawekezaji hao wajenge viwanda nchini na kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa nchini ili kuongeza ajira na pato la Taifa pamoja na kuhakikisha soko la mazao hayo linalotabirika.

Balozi Binaya Srikanta Pradhan alisema India imekuwa na uhusiano mzuri wa kibiashara na uwekezaji na Tanzania hususani katika viwanda vya uchakataji wa mazao ya kilimo, huduma za benki, madini na afya.

Pia alisema India itaendelea kushirikiana na kuendeleza uhusiano wa kibiashara na uwekezaji baina ya nchi hizo pamoja na kuwaunganisha wawekezaji wa Tanzania na India kufanya biashara pamoja.

Alisema wafanyabiashara wa India na Tanzania wanaweza kushirikiana kupitia makubaliano ya kibiashara yaliyopo na maonyesho mbalimbali yakiwemo maonyesho ya kimataifa ya biashara yanayojulikana kama sabasaba.




Mkurugenzi Mtendaji wa benki ya Equity Tanzania, Isabela Maganga (kulia), akiwa na Mkurugenzi wa Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Vya Kati Zanzibar (SMIDA), Soud Said Ali (katikati) na Mkurugenzi wa Wakala wa Uwezeshaji Kiuchumi Zanzibar (ZEEA), Juma Burhani, wakionyesha nyaraka jijini Zanzibar jana, baada ya kutiliana saini makubaliano ya kufanya kazi pamoja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Afutiwa adhabu ya kunyongwa hadi kufa

Na Kulwa Mzee

MAHAKAMA ya Rufani imemfutia adhabu ya kunyongwa hadi kufa Zawadi Fabian na kuamuru shauri hilo la mauaji lianze kusikilizwa upya mbele ya jaji mwingine baada ya kubaini kulikuwa na makosa ya kisheria.

Hukumu hiyo ilitolewa mbele ya jopo la majaji watatu, Ferdinand Wambali, Barke Sehel na Issa Maige walioketi Iringa.

Zawadi alitiwa hatiani na kuhukumiwa kunyongwa hadi kufa na Mahakama Kuu Kanda ya Iringa kwa kosa la kumuua kwa kukusudia Immaculate Mbuligwe Novemba 14, 2019.

Shahidi namba moja, Patricia Mkongwa, alidai siku ya tukio alikwenda kumwona mama yake akiwa na kijana wake lakini hakumkuta nyumbani badala yake alimwona mrufani katika eneo la nyumba ya marehemu iliyoko kijiji cha Limage wilayani Njombe.

Alidai kuwa alimuuliza mrufani aliko mama yake, akajibu amekwenda kwa binti yake lakini alipojitambulisha kuwa yeye ndiye binti yake, mrufani alidai hajui aliko.

Mkongwa alidai kuwa siku ya pili alitoa taarifa kwa mjumbe wa nyumba kumi, Mtendaji wa kijiji na kwa pamoja walikwenda nyumbani kwa Mbuligwe na kukuta wanakijiji wamekaa.

Mrufani inadaiwa alipoulizwa na viongozi alikiri kuua na hata alipopelekwa polisi kuhojiwa, alikiri kwenye maelezo ya onyo kwamba alihusika katika mauaji ya Mbuligwe.

Katika utetezi mahakamani, mrufani alikana kuhusika katika tukio hilo na kudai kwamba alikamatwa kuhusiana na malalamiko ya kuvuta sigara hadharani na si kwa tuhuma za mauaji.

Alidai kuwa alilazimishwa kukiri kufanya mauaji katika maelezo ya onyo, aliteswa, alilazimishwa kusaini nyaraka ambazo hajui ziliandikwa kitu gani.

Baada ya usikilizwaji wa shauri hilo Mahakama iliona upande wa Jamhuri wamethibitisha mashtaka bila kuacha shaka, mrufani akatiwa hatiani na kupewa adhabu ya kunyongwa hadi kufa.

Katika hukumu hiyo mahakama ilizingatia maelezo ya onyo na ushahidi wa mazingira.

Mrufani hakukubaliana na adhabu hiyo, hivyo alipinga akiwa na sababu tatu ikiwamo mwenendo na hukumu ni batili vifutwe na upande wa Jamhuri haukuthibitisha mashtaka dhidi yake.

Wakili Jally Mongo alimwakilisha mrufani na Wakili wa Serikali Mwandamizi Chivanenda aliiwakilisha Jamhuri.

Jopo baada ya kupitia hoja za pande zote mbili, lilikubaliana na hoja moja kwamba mwenendo wa kesi na hukumu ni batili.

"Tunabatilisha mwenendo mzima wa kesi. Mahakama inafuta hukumu na adhabu ya kifo iliyotolewa dhidi ya mrufani. Tunaagiza kwamba kesi dhidi ya mrufani ianze kusikilizwa kwa haraka mbele ya jaji mwingine kwa kufuata matakwa ya sheria na mrufani atabaki rumande.

"Kusikilizwa upya shauri kutawezesha upande wa mashtaka kujaza mapengo kwani ushahidi hautoshi kuthibitisha kesi hiyo," lilisema jopo la majaji.

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



# Waandamana kumpinga diwani madai kufukia kisima cha maji

**Na Vitus Audax,** BUCHOSA

WAKAZI wa Kitongoji cha Nyangalamila B Kijiji cha Nyangalima Kata ya Irenza Halmashauri ya Buchosa wilayani Sengerema mkoani Mwanza, wamefanya maandamano ya amani kumkataa Diwani Mneke Mauna, baada ya kitendo chake cha kufukia kisima cha maji.

Inadaiwa kwamba diwani huyo aliamuru kisima hicho kifukiwe kutokana na kuchimbwa katika kata yake bila idhini yake.

Alipoulizwa kuhusiana na hilo, Diwani Mauna alisema aliamuru mradi huo usitishwe kutokana na kutoutambua kwenye eneo la kata yake. Mauna alisema miradi yote inayotakiwa kutekelezwa katika kata yake ana taarifa zake lakini huo hawezi kukubali uendelezwe kutokana na kutokuwa na taarifa nao.

Mkazi wa Nyangalamila, Ester Msuka, alisema wamekuwa wakitegemea kisima hicho kwa kuwa hali ya upatikanaji wa majisafi na salama katika eneo hilo si nzuri.

"Haiwezekani mtu ambaye ni kiongozi wa wananchi anafukia kisima wanachotakiwa kutumia wananchi wake sio haki kabisa hatumtaki kabisa diwani huyu hana utu," alisema.

Mkazi mwingine, Nchikasi Mashauri, alisema wanakabiliwa na adha ya upatikanaji wa majisafi na kulazimika utumia ambayo si salama kwa afya zao yanayopatikana katika madimbwi.

"Uongozi wa kijiji hicho pamoja na Mbunge wa Buchosa, Erick Shigongo, walichimba kisima hiki ili kitusaidie lakini tunashangazwa na hatua ya diwani kukifukia," alisema.

Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, Fikiri Dotto, alisema wamesikitishwa na kitendo hicho alichofanya diwani huyo kwa kuwa eneo hilo lina tatizo la maji la muda mrefu. Mmiliki wa eneo hilo kilipo kisima hicho, Buyoga Magesa, alisema aliona diwani analeta watu kwa ajili ya kufukia mradi huo kwa maelezo kwamba eneo hilo halifai kuchimbwa kisima cha maji.




Rais wa Catholic Relief Services (CRS), Sean Callahan (katikati), Mkurugenzi wa CRS Kanda ya Afrika Mashariki, Matt Davis (kushoto) na Mkurugenzi Mkaazi wa CRS Tanzania, Kellie Hynes, pamoja wakikata keki kusherehekea miaka 60 ya asasi hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# TAKUKURU yaibua udanganyifu AMCOS

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Pwani imefanya ufuatiliaji kwenye vyama vya ushirika vya msingi vya mazao na masoko (AMCOS) na kubaini uwapo wa udanganyifu katika maeneo mbalimbali.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, Christopher Myava, aliyabainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wakati akitoa taarifa ya miezi mitatu ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi.

Kuhusu uchambuzi wa mifumo, alisema ili kudhibiti mianya ya rushwa katika idara za serikali na sekta binafsi jambo hilo limefanyika kwenye maeneo ya uendeshaji na usimamizi wa masoko ya biashara na utekelezaji miradi kwa kutumia 'force account'.

Alisema uchambuzi huo umefanyika katika AMCOS za Mkongo Kilimani, Kitupa, Nyaminywili, Kipo na Ngorongo zote za wilayani Rufiji.

Myava alisema kuwa katika uchambuzi huo wamebaini kuwepo kwa udhaifu katika utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu za vyama vya ushirika na baadhi ya nyaraka zimekuwa zikitunzwa nyumbani kwa viongozi wa bodi huku akiitaja AMCOS ya Kipo kuwa baadhi ya nyaraka zake zimeonekana kuharibiwa na mchwa.

Alisema hatua ya kukosa kumbukumbu na nyaraka zilizoharibika inasababisha vikwazo kubaini mapato na matumizi takwimu na taarifa za fedha kwa ujumla.

Mkuu huyo wa TAKUKURU alisema katika AMCOS zilizofanyiwa uchambuzi wa mfumo upo udanganyifu wa kutoandika idadi ya kilo sahihi kulingana na mzigo wa mkulima katika upimaji kwa kisingizio cha ubora na unyaufu.

"Mfano mwananchi anafika na kilo 30.5 lakini kwa makusudi ya kufanya udanganyifu wapimaji ambao ni wajumbe wa bodi ya AMCOS watamwambia mkulima mazao yako hayana ubora, hivyo badala ya kilo 30.5 tutakadiria kilo 29.

"Hali hii ikiendelea kwa wakulima zaidi wajumbe hao watajikusanyia kilo nyingi kwa udanganyifu na kutengeneza mauzo kwa majina hewa," alisema.

Myava alibainisha kuwa wananchi wanapobaini udanganyifu huacha kuuza mazao kwenye AMCOS zao na kwenda kuuza kwenye AMCOS za jirani jambo ambalo linasababisha AMCOS mama zinakosa mapato.

Alisema maazimio yaliyowekwa kuwa na ujenzi wa ofisi bora ya kutunza nyaraka na kumbukumbu za ushirika uwe umekamilika ifikapo mwaka 2024, kuandaa taarifa za fedha na kujaza taarifa sahihi katika nyaraka zote za ushirika na kuhakikisha zinatunzwa vizuri.

# Mikumi yajipanga kufikisha watalii 200,000

**Na Joseph Mwendapole**

HIFADHI ya Taifa ya Mikumi mkoani Morogoro, imejiwekea malengo ya kuongeza vivutio mbalimbali ili kufikia watalii 200,000 kwa mwaka kutoka watalii 80,000 wanaotembelea kwa sasa.

Mhifadhi Mwandamizi wa Hifadhi hiyo, Herman Mtei, alisema hayo hivi karibuni wakati wa mafunzo kwa wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari yaliyofanyika mkoani Morogoro.

Mafunzo hayo yaliendeshwa na Chama cha Wanahabari wa Mazingira (JET) na kufadhiliwa na Shirika la Internews Earth Journalism Network East Africa, ambalo pia limewawezesha wahariri hao kutembelea hifadhi hiyo.

Alisema hifadhi hiyo kwa sasa ndiyo inayotembelewa na watalii wengi nchini wakiwamo kutoka nchi za nje na ndani.

Hifadhi hiyo, alisema imetoa ulinzi wa kutosha kwa wanyama wake dhidi ya ujangili ambao alisema umepungua kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Alisema Mikumi pia imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya wananchi kuingiza mifugo ndani ya hifadhi na uzoefu umeonyesha kuwa wengi wao hulipa faini na kurudia makosa mara kwa mara.

"Unakuta mfugaji anatozwa faini ya Sh. 50,000 kwa ng'ombe mmoja lakini haoni shida kulipa faini ya ng'ombe wake wote hata wakiwa 600 kwa sababu anaona ni gharama zilezile ambazo angetumia kuwatafutia nyasi," alisema.

Mtei alisema baada ya kuona wafugaji wamekuwa na tabia ya kuingiza mifugo ndani ya hifadhi licha ya kutozwa faini wameamua kutumia njia nyingine ya kuipiga mnada ili kuacha tabia hiyo.

"Unakuta mtu ana ng'ombe 600 unamtoza faini, analipa, na baada ya muda unamkuta tena na mifugo yake, kwa sababu sheria inaruhusu faini na minada, wakati mwingine tunaona minada ni rahisi kuwafanya wasirudie kuingiza mifugo hifadhini," alisema.

Alitaja baadhi ya maeneo ya uwekezaji katika hifadhi hiyo kuwa ni eneo la Mgoda, Ngotwike Site, View Point, Mke Mgumba Site, Campsite Namba 5 na Chogawale.

Mtei alisema katika hifadhi hiyo kuna sehemu nzuri ya kuona ndege wa aina 400 wakiwamo korongo na kwamba watalii wanashiriki uzoefu kutoka kwa vijiji vilivyo karibu na bustani kama vile kupika chakula na kucheza.

Alisema pia wamewekeza katika utalii wa mikutano na kuna vyumba vya kufanyia matukio mbalimbali kama vile mikutano rasmi, warsha na semina.

Alizitaja shughuli za utalii ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi kuwa ni utalii wa mchana na kusema kuwa hiyo ndiyo shughuli kuu katika hifadhi hiyo kwa ajili ya kufurahia wageni.

"Utalii wa kupika na porini ni ulimwengu tofauti kabisa wakati wa usiku hii ndiyo inafanya safari ya usiku kuwa maalum na safari ya kutembea ambapo hufanyika katika njia maalum za kutembea, ambapo wageni hufurahia uhisia katika nyika," alisema.



## Viwanja vya ndege Arusha, Moshi kushindana kibiashara

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

USHINDANI wa kibiashara kati ya Uwanja wa Ndege wa Arusha na Moshi, 'utaamua' aina ya ndege zitakazoruhusiwa kutua katika viwanja hivyo, baada ya serikali kutenga zaidi ya Sh. bilioni 12.344 kupanua Uwanja wa Ndege wa Moshi ili kuwavutia mawakala na watalii kuutumia uwanja huo.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kuamua kuuboresha uwanja huo ni kutaka kuimarisha usafiri wa anga kwa ajili ya kuinua pato la taifa kupitia sekta ya utalii.

"Huu mradi unatekelezwa hivi sasa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), chini ya usimamizi wa Meneja wa Mkoa wa Kilimanjaro. Thamani ya mradi huu hadi kukamilika ni bilioni 12.344 na serikali imetoa kwa awamu ya kwanza Sh. bilioni 1.851," alisema.

Utekelezaji wake unahusisha ujenzi wa eneo la usalama (runway strip), lenye upana wa mita 75 kila upande kwa njia kubwa (main runway) pamoja na eneo la mita 40 kila upande wa njia ya pili.

Kazi nyingine ni ujenzi wa barabara mbili za mchepuo wa ndege (taxiway), yenye urefu wa mita 62.5 na upana wa mita 18. Yamo pia maboresho ya maegesho ya ndege (apron), yenye urefu wa mita 140 na upana wa mita 59.

Aidha, alizitaja kazi nyingine kuwa ni ujenzi wa barabara ya kuingia na kutoka uwanjani (mita 520) kwa kiwango cha matabaka mawili ya lami na kuweka uzio wa usalama katika uwanja.

Vilevile, TANROADS itatekeleza mradi huo kwa kutengeneza barabara ya mzunguko ndani ya uwanja yenye urefu wa mita 8,000 kwa kiwango cha changarawe.

Babu, alisisitiza kuwa kwa sasa, mradi huo uko katika hatua ya utekelezaji na umefikia asilimia 15.

Idadi ya watalii wanaotembelea Mkoa wa Kilimanjaro kutoka ndani na nje ya nchi, imeendelea kuongezeka kutoka watalii 4699 mwaka 2020 kabla ya filamu ya 'The Royal Tour' hadi kufikia watalii 61,801 mwaka 2022.

# Kibong'oto kutoa madaktari kuongeza nguvu kudhibiti Marburg

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKURUGENZI wa Hospitali Maalum ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto, Dk. Leonard Subi, amesema licha ya kutokuwapo ongezeko la wagonjwa walioambukizwa virusi hatari vya Marburg, amewaweka tayari madaktari watatu watakaongeza nguvu kwenye jopo la wataalamu waliopelekwa na Wizara ya Afya, mkoani Kagera, iwapo watahitajika.

Akizungumza jana na vyombo vya habari kuhusu ugonjwa huo, Dk. Subi, alisema timu yao iko tayari kwa ajili ya kukabiliana na udhibiti wa ugonjwa huo, ambao hauna tiba mahususi, bali hutibiwa kwa dalili anazokuwa nazo mgonjwa.

"Tulibainisha madaktari watatu kwenda Kagera, baada ya kuwa tayari wengine wameshaenda kule na sasa hivi hatujaona ongezeko la wagonjwa ila timu yetu iko standby (iko tayari).

"Kwahiyo sisi tunakaa standby na timu yetu, lakini na kule wako standby, kwa hiyo huwa tunaendelea kujifua."

Kwa mujibu wa Dk. Subi, ugonjwa huo huambukizwa kutoka kwa binadamu mmoja kwenda kwa mwingine, kwa njia ya kugusa majimaji ambayo yanaweza kuwa mate, mkojo, damu, machozi au kinyesi yatokayo kwenye maiti au mgonjwa mwenye dalili.

Alisisitiza kuwa maambukizi yake pia yanaweza kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu, iwapo mtu atakula au kugusa mizoga au wanyama walioambukizwa.

Machi 16, mwaka huu, Wizara ya Afya nchini, ilitangaza uwapo wa ugonjwa usiojulikana katika Wilaya ya Bukoba Vijijini, Kata ya Maruku na Kanyangereko katika vijiji vya Bulinda na Butayaibega, ambao uliwaua watu watano na wengine watatu kupata maambukizi.

Naye Dk. Lilian Mahemba, akifafanua zaidi kuhusu ugonjwa huo, alisema mtu yeyote mwenye dalili za homa, kutapika, kuharisha, kutoka damu na mwili kuishiwa nguvu anashauriwa kuwahi kituo cha kutolea huduma za afya mapema kwa ajili ya uchunguzi na matibabu.

Miongoni mwa waliofariki dunia kutokana na ugonjwa huo ni Benson Rutabingwa, ambaye alielezwa na kaka yake, Reskipius Rutabingwa, kwamba alitarajiwa kufunga ndoa mwezi ujao.

Huu ni mlipuko wa kwanza nchini, lakini nchi kadhaa za Afrika zimewahi kuripoti mlipuko wa virusi hivi, ikiwamo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Kenya, Afrika Kusini, Uganda na Zimbabwe.

Virusi vya Marburg vinatajwa na wataalamu wa afya kwamba ni sawa na virusi hatari vya ebola, viligunduliwa kwa mara ya kwanza mwaka 1967 nchini Ujerumani, baada ya watu 29 kuambukizwa na saba kufariki dunia.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera, akizungumza na madiwani na watumishi wa Halmashauri ya wilaya hiyo jana, kuhusu wakulima kuhifadhi mazao kupitia mpango wa stakabadhi ghalani. **PICHA: GIFT THADEY**

# Zaidi wanafunzi 500 darasa la 1 wagundulika hawajui KKK

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WANAFUNZI 512 wa darasa la kwanza mkoani Manyara, sawa na asilimia 19, kwa mwaka uliopita, waligunduliwa hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu.

Akizungumza na Nipashe jana katika mahojiano maalum, Ofisa Elimu Taaluma wa Mkoa huo, Julitha Akko, alisema baada ya serikali kugundua hilo, walitumia mbinu mbalimbali kuhakikisha wanafunzi hao hawavuki kuingia darasa la pili hadi wajue kusoma, kuandika na kuhesabu.


"Faraja kubwa kwetu ni kwamba, hadi kufikia katikati ya mwaka 2022 kulikuwa na tatizo hilo, lakini baadaye tulifanikiwa na tumepambana mpaka wamejua kusoma, kuandika na kuhesabu. "Unajua mwaka jana mkoa uliandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza 48,379 wakiwamo wavulana 24,614 na wasichana 23,763."

Aidha, Akko, alisema chanzo cha wanafunzi kushindwa kujua kusoma, kuandika na kuhesabu ilikuwa ni msongamano wa wanafunzi darasani ila baada ya serikali kujenga madarasa ya kutosha tatizo hilo limeisha.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, hivi sasa serikali inatumia mfumo wa 'key performance indicator' ambao ni kila baada ya muda wa miezi mitatu, wanafunzi wanapewa mitihani ya upimaji.

"Kwa wanafunzi ambao wamepita darasa la awali, hawana shida na shule zote za msingi zina madarasa ya awali na kila shule ina mwalimu wa awali,"alisisitiza.

Januari 13, mwaka huu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angela Kairuki, alipiga marufuku wanafunzi wa darasa la kwanza kupanda darasa, bila kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.





# Watendaji wafundwa usimamizi rasilimali

**Na Marco Maduhu,** MARA

WATENDAJI wa Kata na Mabaraza ya Kata Wilaya ya Butiama mkoani Mara, wamepewa mafunzo ya mfumo wa ufuatiliaji wa uwajibika kwa jamii na utawala bora, katika kuhakikisha wanasimamia rasilimali za nchi na utunzaji wa mazingira.

Mafunzo hayo yalitolewa juzi na Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa vitendo, Lawyers Environment Action Team (LEAT), ambayo yatadumu siku tano kwa Watendaji na Mabaraza ya Kata ambao wanatoka katika maeneo ya uchimbaji madini.

Mkufunzi wa mafunzo hayo, Hana Lupembe kutoka (LEAT), alisema viongozi hao wakipewa elimu hiyo ya mfumo wa ufuatiliaji wa uwajibikaji kwa jamii na utawala bora, itawasaidia katika utendaji wao kazi kwa wananchi, na kufanya vyema katika usimamizi wa Rasilimali za nchi na kuzuia uharibifu wa mazingira katika uchimbaji madini.

"LEAT tunatoa mafunzo haya kwa viongozi kuanzia ngazi za chini ili wakawe watendaji wazuri na kuwajibika katika kusimamia rasilimali za nchi katika sekta ya uchimbaji madini na kuzuia uharibifu wa mazingira," alisema Lupembe.

Valeria Macha kutoka (LEAT), alisema licha ya kutoa mafunzo ua utunzaji wa mazingira, pia wanawajengea uwezo wananchi na viongozi wanaoishi katika maeneo ya uchimbaji wa madini kujua haki zao za msingi, pamoja na kurudisha uoto wa asili baada ya uchimbaji na kuhamia eneo jingine ili kuzuia uharibifu wa mazingira.

Ofisa Usimamizi wa taka na usafi wa mazingira Wilaya ya Butiama, Karani Ruhumbika, aliwataka viongozi hao kila mmoja katika eneo lake kuwa na wajibu wa kutunza mazingira, pamoja na wananchi kufanya uchimbaji wa madini uwe salama bila ya kuathiri mazingira.

Baadhi ya watendaji wa kata Wilaya ya Butiama ambao wanatoka kwenye maeneo ya uchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu, walisema mafunzo hayo yatakuwa chachu ya uongozi wao na kuongeza uwajibikaji katika majukumu yao, pamoja na kusimamia vyema rasilimali za taifa na utunzaji wa mazingira.

# Biteko azitaka kampuni kuwainua wachimbaji wadogo

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

WAZIRI wa Madini, Dk. Doto Biteko, amezitaka kampuni kubwa za uchimbaji madini pamoja na taasisi zinazojihusisha na masuala ya madini kuwasaidia vifaa wachimbaji wadogo wanawake na watu wenye uhitaji maalum ili kuwainua kiuchumi katika shughuli zao za uchimbaji.

Waziri Dk. Biteko alitoa kauli hiyo juzi mkoani Geita wakati akishuhudia utiaji saini wa mkataba wa kandarasi ya uchorongaji miamba wa miaka miwili 2023 na 2024 baina ya Shirika la Taifa la Madini (STAMICO) pamoja na GGML.

Kadhalika shughuli hiyo iliyoambatana na kukabidhi vifaa kwa wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu wenye usikivu hafifu vilivyotolewa STAMICO vyenye thamani ya Sh. milioni 8.6.

Dk. Biteko alisema hatua hiyo itawasaidia wachimbaji hao kupiga hatua kiuchumi na kulipa kodi ya serikali kwa wakati, huku akizitaka kampuni na taasisi nyingine kuiga mfano kwa shirika hilo katika kuwasaidia wachimbaji hao wenye uhitaji.

Aidha, Dk. Biteko aliutaka uongozi wa shirika hilo kuwa wakali kwa baadhi ya watumishi wao wasio waadilifu na kuwachukulia hatua kali za kisheria ili kudhibiti vitendo vya ubadhirifu katika shirika hilo.

Alisema kuwa kazi kubwa ya STAMICO ni kuwezesha kimkakati miradi ya mnyororo wa thamani wa madini kwa niaba ya serikali ili kuwawezesha wachimbaji wadogo ambao kwa sasa wamekuwa na mafanikio makubwa wanajiendesha tofauti na hapo awali.

Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO, Dk. Venance Bahati Mwasse, alisema vifaa hivyo vitawasaidia wachimbaji hao kuinua uchumi na kuongeza mnyororo wa thamani wa madini na kuwa na uhakika wa kufanya kazi zao.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa mgodi wa dhahabu Geita GGML, Damon Elder alisema; "tuliingia kandarasi kwa mara ya kwanza mwaka 2020, leo tena tumesaini mkataba wa kandarasi ya uchorongaji miamba kwa miaka miwili 2023 na 2024 tunaahidi kuendeleza ushirikiano mzuri katika kuendesha shughuli zote za uchimbaji.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Geita, Cornal Magembe, aliyehudhuria hafla hiyo ya utiaji saini mkataba wa kandarasi ya uchorongaji miamba kati ya STAMICO na GGML alisema analipongeza Shirika la Madini la Taifa na

GGML na mkataba huu utakuwa na matokeo chanya kwa Wanageita na taifa kwa ujumla.



Mkazi wa Mtaa wa Nyakato, Kata ya Nyasubi, Peter Masunga, akiokota nguo za watoto wake baada ya kubomolewa nyumba yake na dalali wa Mahakama ya Ardhi Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga jana, kupisha kiwanja namba 402 kinachodaiwa kumilikiwa na Taasisi ya Kidini ya Kiislamu ya "Kahama Muslimu Center". **PICHA: SHABAN NJIA**

# Vijiji 70 vyaunganishiwa umeme Sengerema

**Na Elizabeth Seleman** SENGEREMA

VIJIJI 70 na vitongoji 194 katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza vimefikiwa na huduma ya umeme, kati ya vijiji 72 na vitongoji 421 vilivyo katika mpango wa kupatiwa huduma hiyo sawa na asilimia 98.6.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Shirika la Umeme Nchini (TANESCO) wilayani hapo, Martine Kilenga na kubainisha kuwa asilimia kubwa ya vijiji vimefikishiwa huduma ya umeme na kazi hiyo inaendelea.

Aidha, alisema katika Halmashauri ya Sengerema kuna visiwa sita ambavyo vinapatikana kata ya Katunguru na Chifufu maeneo hayo umeme utaunganishwa kupitia mfumo wa REA na kuwaondoa hofu wananchi wa maeneo hayo. Kadhalika alisema utaratibu wa kulipia umeme kwa bei ya 27,000 bado uko palepale huku akiwaomba wateja ambao hawajaunganishiwa wawe na subira kwa kuwa nguzo za umeme zinatarajiwa kuwasili katika wilaya hiyo mwishoni mwa mwezi Machi.

Kilenga alisema kwa sasa Wilaya ya Sengerema imepokea msimamizi wa REA kutoka serikalini ambaye atajihusisha na mambo ya REA katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

ama
ALHAMISI MACHI 30, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**Wauguzi wakiri kuna 'vishoka' kati yao, waamua kupambana nao**



Ukurasa 13

Wanamazingira wathibitisha uwezekano kurejeshea Milima Uluguru kijani cha miti



Ukurasa 12

**Rais katika miaka miwili akibeba ushuhuda wa kukomboa mtoto**

KUTOKA DODOSO LA KILELE...

# Miaka miwili Awamu ya Sita, wiki iliyosheheni uzinduzi miradi maji

**Na Frank Monyo**

Ni wiki iliyobeba matukio ya kuzinduliwa miradi mingi ya maji, ambayo ni sehemu ya kusherehekea kutimu miaka mwili ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan madarakani, kilele kilikuwa siku 13 zilizopita.

Pia, kuna mengi yamenenwa kuhusu tija na mazuri anayoyawajibikia ofisini, yakiakisi mafanikio ya utumishi wake kwa umma, ambayo sekta ya maji haikusahaulika, ikizingatiwa mwenye cheo ni mwanamama, hivyo ' ndoo ya maji kwa mama kichwani, imepata mtuaji.'

Kiutendaji, ufunguo wa jukumu hilo kapatiwa Waziri kijana, Jumaa Aweso, aliyekwisha onywa tangu mwanzo wa safari, 'akimzingua' (Rais), naye atazunguliwa.' Hivyo, katika kukwepa 'kuzinguliwa' hana masihara, yuko 'damudamu' na kaulimbiu 'kazi inaendelea.'

Sura ya sekta ya maji ikajitokeza kwenye kilele, pale katika wiki hiyo ikiwa na miradi 22 yenye thamani zaidi ya Sh. bilioni 133 inazinduliwa, ikitarajiwa kuhudumia zaidi ya watu milioni 1.2.

Pia, kunatajwa kuwapo miradi tisa yenye thamani zaidi ya Sh. bilioni tisa, sasa imeshawekewa mawe ya msingi.

### ATUA NDOO TEGETA

Ilikuwa Alhamisi ya Machi 16, siku tatu tu kabla ya kutimu chereko, Rais Dk. Samia na miaka miwili katika uongozi, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, anashuhudiwa akizindua mradi wa maji Makongo hadi mji wa Bagamoyo, ambayo inazindua rasmi Wiki ya Maji, kukitarajiwa wanufaika 450,000.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (kushoto), wakizindua Mradi wa Ujenzi wa Mfumo wa Maji kati ya Makongo mkoani Dar es Salaam na Bagamoyo mkoani Pwani, ikiendana na Wiki ya Maji, kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Tegeta, tarehe 16 mwezi huu. Wa pili kushoto ni Kaimu Mwakilishi Mkazi wa Benki ya Dunia nchini, Peetri Arora na kulia, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Kiula Makala Kingu. **PICHA: MTANDAO**

Mantiki yake ni mradi uliosubiriwa kwa muda mrefu na wakazi wa Dar es Salaam; Tegeta A, Mivumoni, Goba, Madale na Wazo, wakikosa huduma hiyo ya maji kwa muda mrefu.

Waziri Mkuu anawaambia: "Serikali inatambua changamoto ya maji iliyokuwapo kwenye maeneo haya, na ndio maana Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alifanya uamuzi wa dhati kusukuma utekelezaji wa mradi huu, ili wananchi mpate maji.

"Serikali kwa pamoja inaendelea na jitihada mbalimbali za kutafuta vyanzo mbalimbali vya maji, ili kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi wote."

Rai yake ni haja ya kuwa makini na kutokukubali umma kuwalaghai au dai la rushwa kwa ajili ya kuunganishiwa maji, akihimza utaratibu wa serikalii kuunganisha watu maji uzingatiwe.

Anaongeza: "Niwatake wananchi kuwa na tabia ya kulinda na kutunza vyanzo vya maji pamoja na mazingira, kuharibu mazingira ni kuhujumu."

### JIJINI DODOMA

Waziri Aweso ana utangulizi, serikali kutambua changamoto ya upatikanaji huduma ya maji kwa wakazi wa jijini Dodoma kutokana na ongezeko kubwa la watu baada ya makao makuu ya serikali kuhamia hapo, hivyo kuna ongezeko la shughuli za kiuchumi na kijamii.

Kwa mujibu wa Aweso, mahitaji ya majisafi jijini Dodoma yanakadiriwa kuwa lita milioni 133.8 kwa siku, wakati uzalishaji kutoka katika vyanzo vyote ni lita milioni 66.7 kwa siku. Hivyo, kuna upungufu wa maji katika jiji la Dodoma kwa takribani lita milioni 67.1. Huo upungufu zaidi ya kiwango cha uzalishaji, kwa maana ya asilimia 50.2.

### SAME-MWANGA-KOROGWE

"Katika miradi mirefu na ya siku nyingi, inatengenezwa na kusita na kusimama ni Same-Mwanga - Korogwe, tunakwenda kutafuta fedha, tuhakikishe unatekelezwa na watu wapate maji," anatamka Rais Dk. Samia.

Huo ni ufafanuzi wake Juni mwaka jana, akiuelezea mradi uliokwama kwa muda mrefu, sasa akifufua matumaini ya kupata majisafi, salama kwa wananchi zaidi milioni moja, ukitarajiwa kugharimu Sh. bilioni 262 hadi kukamilika.

Alipoingia madarakani Machi 2021, Rais Dk. Samia akaukuta mradi huo una uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 65 kutoka Bwawa la Nyumba ya Mungu ukikabiliwa na changamoto za kisheria na kifedha, akafanikisha kutatua na ulipaswa kukamilika mwaka huu.

INAENDELEA UK.12

AFYA

## KUTOKA DODOSO LA KILELE...

# Rais katika miaka miwili akibeba ushuhuda wa kukomboa mtoto

**Na Beatrice Shayo**

• Hatua za usalama, afya yake shule hadi nyumbani



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Sasha Joseph Mbilinyi, mtoto wa mwanasiasa ambaye ni msanii wa Hip-hop, Joseph Mbilinyi 'Sugu', katika tamasha la Dream Concert, lililofanyika Serena jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

HAINA siku nyingi kusikika agizo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ikitaka wanafunzi wa elimu ya msingi wa kuwa bwenini, ni kuanzia darasa la tano, agizo litakaloanza kutekelezwa Juni ijayo, sambamba na vigezo maalum kwa magari ya shule yanayosafirisha wanafunzi katika namna ya kuwahudumia.

Inapoangaliwa kwa undani katika kutimiza miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, anataja hilo la kuzuia wanafunzi wadogo kuwa bwenini. Pia, anataja la kurejeshwa shuleni wanafunzi waliopata ujauzito.

Ikirejewa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008, inaainisha haki tano za msingi za mtoto ambazo ni za kuishi, kulindwa, kuendelezwa, kushiriki na kutobaguliwa.

Mnamo Novemba mwaka 2021 aliyekuwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Joyce Ndalichako, katika mafanikio ya miaka 60 ya uhuru wa nchi, chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia, akatangaza wanafunzi waliokatisha masomo kwa kupata mimba, wataruhusiwa kurejea shuleni baada ya kujifungua.

### MARUFUKU BWENINI

Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, mnamo tarehe 5 mwezi huu, akaagiza shule zote zinazotoa huduma ya bweni kwa madarasa ya awali hadi la nne, kusitisha huduma hiyo ifikapo Juni ijayo.

Ni waraka aliyoutoa kwa vyombo vya habari, ukifafanua; "Maendeleo ya kweli katika nchi yoyote ile, kwa kiasi kikubwa hutegemea ubora wa elimu, inayotolewa katika nchi husika, ingawa dhana ya ubora wa elimu hutofautiana kutoka nchi moja, hadi nyingine katika muktadha wa nchi yetu."

Anafafanua kuwa elimu bora ni inayomjengea mhitimu uwezo wa kuchambua mambo kwa ufasaha, ili kufanya uamuzi wenye tija, kuwa na maadili yanayoakisi mila, desturi na utamaduni, akijenga moyo wa kupenda, kuthamini na kufanya kazi ili kuleta maendeleo ya mtu binafsi, jamii na taifa kwa ujumla.

Dk. Mtahabwa anasema kuna makambi mengi yamebainika kuwa na mazingira hatarishi kimaadili, usalama na afya za wanafunzi, pia yameanzishwa bila ya kufuata taratibu rasmi za kuanzishwa mabweni au makazi ya pamoja ya wanafunzi.

Hapo anasisitiza kuwa malezi na makuzi ya mtoto mara zote yanategemea mchango wa familia kupitia wazazi au walezi, huku kukibainika kuwapo baadhi ya shule zinazopokea watoto wenye umri mdogo kuanzia darasa la awali hadi la nne, pasipo kuzingatia taratibu stahiki.

"Huduma za bweni kwa wanafunzi wenye umri mdogo ikiwamo wa elimu ya awali na darasa la kwanza hadi la nne, huwanyima watoto fursa ya kushikamana na familia na jamii zao, kujenga maadili na kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya familia na jamii zao," anasema.

Anarejea tafiti zinaonyesha kuwapo madhara ya muda mrefu, yatokanayo na kulaza watoto bwenini katika umri mdogo, wakikosa mapenzi ya wazazi na walezi, hata wanashindwa kuwa sehemu ya familia na jamii husika.

Msomi Dk. Mtahabwa, anasema kilichoamuliwa ni utekelezaji wa mwongozo wa uanzishaji na usajili wa shule uliotolewa na wizara hiyo, Novemba mwaka 2020.

Anaainisha zaidi:"Hairuhusiwi kwa shule yoyote ile kuwa na makambi ya kitaaluma. Hatua hii inaakisi utekelezaji wa Waraka wa Elimu namba tatu wa mwaka 2007 kuhusu kukataza kambi za masomo katika shule za msingi."

### KUFICHULIWA UKATILI

Mwaka jana, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akawataka watoto kote nchini kufichua viashiria vya ukatili dhidi yao, maendeleo ya shuleni na majumbani.

Waziri Dk. Gwajima, amewasisitiza watoto wasihofie kuweka wazi, pale waonapo viashiria vya ukatili na kutoa taarifa kwa watu wanaowaamini, ikiwapo dawati la jinsia kwenye vituo vya polisi.

Anarejea takwimu za matukio ya ukatili kwa watoto katika kipindi kati ya Januari hadi Desemba mwaka 2021, kwamba, matukio yaliyoripotiwa kwa Jeshi la Polisi yalikuwa 11,499, ikilinganishwa na matukio 15,870 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

Ufafanuzi wake ni matukio 4,371 kupungua, sawa na asilimia 27.5

Mikoa iliyoongoza wakati huo ilikuwa; Arusha (808), Tanga (691), Shinyanga (505), Mwanza (500) na Mkoa wa Kipolisi Ilala (489) na aina ya makosa yaliyoongoza kwa idadi ni ubakaji; 5,899, mimba kwa wanafunzi 1,677 na ulawiti 1,114.

### KUTOKOMEZA UKEKETAJI

Wizara tajwa kwa kushirikiana na wadau imeandaa Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji wa Mwaka 2020/21 kutokomeza ukeketaji ifikapo 2024/25.

Waziri Gwajima anafafanua kwamba, ukeketaji una madhara makubwa kiafya, kisaikolojia, kusababisha kuvunjika ndoa na watoto kukosa malezi. Mikoa yenye takwimu za juu za ukeketaji hadi wakati huo na kiwango chake kwenye mabano ni: Manyara (58%), Dodoma (47%), Arusha (41%), Mara (32%) na Singida (3%).

Waziri anasema katika vita kukabili ukeketaji kwenye mikoa mbalimbali, jumla ya ngariba 1,800 walioamua kuachana na vitendo hivyo, kati ya mwaka 2015/16 hadi Aprili, 2022.

### MABARAZA YA WATOTO

Wizara hiyo ikatoa miongozo ya Mabaraza ya Watoto na kuanzishwa madawati ya watoto katika shule za msingi na sekondari, ikitajwa ni hatua muhimu kukabiliana na kadhia ya ukatili.

Hadi sasa watoto nchini, wamekuwa wakipitia ukatili mbalimbali ikiwamo ya mitandaoni, hivyo serikali kwa kushirikiana na wadau, imeshaandaa miongozo kwa wanafunzi, walimu na wazazi iwe msaada katika malezi na makuzi ya watoto.

Ni hatua inayoshuhudiwa na marejeo ya Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008, inayotambua haki tano za msingi za mtoto, ambazo ni haki za: Kuishi, Kulindwa, Kuendelezwa, Kushiriki na Kutobaguliwa, hivyo kuzinduliwa mwongozo wake, ni chachu muhimu katika kuongeza mapambano ya kumlinda mtoto huyo.

Hadi sasa, kuna miongozo inayopelekwa kwenye shule za msingi na sekondari, pia vyuo vya kati, kwenye madawati ya ulinzi wa mtoto na mabaraza ya watoto yanayoenda kuanzishwa nchi nzima, ili kuwa fursa kwao kujadiliana na kueleza madhila yanayowasibu.

Serikali na wadau baada ya tafiti zake, waliona umefika wakati watoto kupatiwa miongozo itakayowasaidia kuendesha wa mabaraza yao, huku wazazi na walezi kote nchini, wakitakiwa kuwaruhusu watoto kujiunga na kushiriki katika mabaraza yao, itakayowapa fursa kwao, kubainisha changamoto zinazowakabili.

## Miaka miwili Awamu ya Sita, wiki iliyosheheni uzinduzi miradi maji

**INATOKA UK.11**

Waziri wa Maji, Aweso anawataka makandarasi wa Mradi wa Maji wa Same-Mwanga-Korogwe kukamilisha kazi zilizosalia katika mradi huo akiwapa miezi 14 na kusisitiza mkandarasi asiweke sababu za kukwama.

Pia, akawaahidi viongozi wa wizara yake watafanya kazi usiku na mchana, kumwelekeza mkandarasi kuweka ratiba ya mpango kazi hadi kukamilisha mradi.

### MAMA AKIWA ARUSHA

Mnamo Oktoba 2021, Rais Samia akiwa Arusha, akasema serikali imeshatoa Sh. milioni 520 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji jiji humo na baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Arumeru.

Anafafanua alipokuwa kijijini Chekereni, akizungumza na wana - wilayani Arumeru, baada ya kukagua mradi wa maji kwenye kisima cha mashine ya kusukuma cha maji, Rais Dk. Samia, akawaahidi serikali inaendelea kutatua changamoto zao za maji mkoani Arusha, na shida zao zitakwisha, pale mradi huo mkubwa utakapokamilika.

MAZINGIRA

# Wanamazingira wathibitisha uwezekano kurejeshea Milima Uluguru kijani cha miti

• Ajenda 'mtaa kwa mtaa' Moro yote

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MKOANI Morogoro penye shirika lisilo la kiserikali linalojihusisha na usimamizi wa mazingira (AGRIWEZESHA) kuna bosi wake mkuu, Mkurugenzi, Degrasia Ignas, anayesema wakati umefika kwa jamii kupanda miti na kuipenda, ili kuisimamia katika makuzi na hata kuona faida yake baadaye.

Anasema katika shughuli zake, amelazimika kuweka kaulimbiu 'panda mti penda mti 'ili kuleta hamasa kwa jamii kupenda miti wanayoiona, iwe wameipanda au wameikuta, kwa sababu mtu akipenda kitu ni lazima akitunze.

Ignas anahamasisha kuwa, ni aina ya kaulimbiu inayoleta maana katika utunzaji misitu na mazingira kwa ujumla kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Mkuu huyo anasema, kupitia mradi huo uitwao Agroforestry uliofadhiliwa na Taasisi ya Reforestaction kutoka Afrika Kusini, wamepanda miti ambayo jamii inapaswa kuipenda, mimea hiyo nayo inarejeshe manufaa ya kumtunza binadamu kwa faida za kuivuna, kuuza, huku wakipata hewa safi, upepo na kivuli.

Ignas anasema hadi sasa wameshapanda miti zaidi ya 7,000 katika vijiji vyote vya tarafa ya Mgeta mkoani Morogoro, ikiwamo kwenye eneo la hifadhi asilia ya milima ya Uluguru, katika kijiji cha Nyandira.

Hiyo ni sehemu ya mradi mkubwa wa upandaji miti unaohusisha kilimo mseto, kwa upandaji miti na mazao hasa kwenye mashamba ya wakulima ndani ya mipaka ya vijiji vya Nyadira na Chenzema.



Wanakijiji wa Nyandira, Tarafa ya Mgeta, wilayani Mvomero, wakiimba nyimbo za utunzaji misitu na mazingira, wakiwa na miche ya miti kwa ajili ya kuipanda. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

**Nimepanda miti kwa kung'oa kutoka maeneo mbalimbali kabla ya ujio wa Agriwezesha. Vijana wamenivizia na kuiba kwenda kuuza, kwa sababu hawataki kujituma, vizazi vijavyo vitanufaika na nini sasa?**

### MALENGO YALIVYO

Mkurugenzi huyo anasema taasisi hiyo iliyoanzishwa Agosti 2019 inatarajia kupanda miti 440,000 ifikapo mwaka 2025, ili kuboresha utunzaji wa mazingira na misitu kwa ujumla.

Anasema, kwa kushirikiana na wakazi husika, wameshapanda miti ya asili, matunda na ya mbao, kwa kuzingatia maeneo yamo hifadhini, wakulima na wadau wengine wa misitu.

Kwa mujibu wa Ignas, hado sasa wamejikita wilayani Mvomero tarafa ya Mgeta, akitaja kwenye vijiji 11, ambavyo ni; Pinde, Tandali, Nyandira, Chenzema, Langali, Maguruwe, Lukunguni, Kibaoni, Vinile, Bunduki na Kibigili na vijiji vya kata ya Lubungo.

Hapo anaeleza imani yake kwamba, kazi imeshafanyika na itaacha alama kubwa katika Milima ya Uluguru, ambayo haitafutika kwa vizazi vingi.

Ignas anasema, wanauendesha mradi sambamba na kutoa elimu kwa makundi ya kijamii, ikijumuisha wanufaika ambao ni wakulima, katika namna ya kuanzisha vitalu na kukuza miche hadi kufikia upandaji, sambamba na kuwaelimisha watoto na wanafunzi elimu hiyo kusaidia vizazi vijavyo.

Anasema lengo kubwa la kazi ya asasi hiyo, ni kueneza elimu na itikadi ya jamii, kuhusu umuhimu wa kupanda na kulinda miti, kazi ambayo imeshawafikia wakazi wanufaika 3000, kwa matarajio watakuwa wasimamizi endelevu wa misitu.

Matarajio ya Agriwezesha, inataja ni kuhamia wilaya nyingine za mkoa Morogoro, kueneza elimu hiyo ili kutimiza dhana ya utunzaji misitu na uhifadhi wa mazingira katika miradi mbalimbali ya umma, itakayosaidia jamii kushiriki kulinda na kuisimamia misitu waliko.

Mkurugenzi Ignas anasema, miti yote waliyopanda wameingiza kwenye mfumo wa ufuatiliaji na wataalamu wao wanafanya kazi na wakulima na wahifadhi misitu, kufuatilia changamoto zinazoweza kujitokeza, ili washiriki kuzitatua kwa wakati.

"Nawaasa vijana kujenga tabia ya kupenda mazingira na misitu, kwa kuzingatia kaulimbiu ya Agriwezesha inayosema 'Panda Miti, Penda Miti.' Kwa vijana naomba watambue ili tuweze kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, njia mojawapo ni kulinda misitu tuliyo nayo na kupanda miti zaidi.

"Tuondoe dhana ya kwamba, upandaji wa miti ni kazi ya wazee, vijana ni nguvu kazi ya taifa pia tuchukua hatua tuwekeze nguvu zetu kwenye utunzaji wa mazingira," anasema.

### OFISA MISITU

Ofisa Msitu Msaidizi wa Hifadhi ya Mazingira asilia Uluguru, Edson Jackson, anasema upandaji miti ni neema kwa jamii, kwenda kufaidi matunda ya ukuaji misitu baadaye.

Anaasema, hali ya uhifadhi msitu Uluguru iko vizuri, kwa sababu ya uangalizi bora na wa kila mara, sambamba na kuendelea kutoa elimu ya moto na utunzaji mkubwa wa mazingira, vyote vikifanya milima hiyo ionekane bora wakati wote.

"Usiridhike kumuona mtu ameingia msituni kukata mti. Huyo anakuharibia vitu vingi sana, kwa sababu kukata mti mmoja ni kuharibu oksijeni ya watu karibia 1,000, hivyo tuwe mabalozi, lakini tuhimize uhifadhi kwa maeneo yetu na vizazi vinavyokuja," anasema.

### WENYEJI WAFUNGUKA

Mzee Fridolin Kurunge (78), mkazi wa kijiji cha Nyandira, Tarafa ya Mgeta, anasema mazingira yameanza kubadilika na kuwa mazuri kwa sababu ya Agriwezesha kupanda miti katika tarafa yao, ambayo haikuwa na miti kabisa.

Anaeleza masikitikio yake kwa tabia za vijana kutojituma kupanda miti, badala yake wanaangukia kuzurura mitaani na kuvuna miti ya wenzao waliyopanda, hali inayorudisha nyuma mipango ya wenzao kimaendeleo.

Mzee huyo anaendelea: "Angalia hata sasa na uzee wangu huu, nimehusika kuingia kwenye kitalu hiki, kwa sababu nimeona uchungu sana, mti una faida kubwa sana na unaleta manufaa mengi sana. Vijana wapo badala ya kutunza wao ni mojawapo ya uharibifu wa mazingira.

"Nimepanda miti kwa kung'oa kutoka maeneo mbalimbali kabla ya ujio wa Agriwezesha. Vijana wamenivizia na kuiba kwenda kuuza, kwa sababu hawataki kujituma, vizazi vijavyo vitanufaika na nini sasa? Mbona wazee wetu walikuwa wanatuachia urithi wa kujituma na tunaitikia," anahoji Mzee Kurunge.

Hapo anaiomba serikali kuhamasisha vijana zaidi kuiga mfano wa wazee walivyofanya zamani, ili kuwa na mwamko wa kupanda miti na kuipenda miti kama kaulimbiu ya upandaji miti ya Agriwezesha inavyotamka.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Wapanda Miti kwenye vitalu Kijiji cha Maguruwe, Maria Mkwama, analalamika kinamama wanahangaika kutafuta kuni za kupikia majumbani, nao sasa wamehamia kupenda mti, ili kujikwamua na magumu hayo.

Mama huyo anasema, mpaka sasa wamewachukua vijana wakiwamo wa kike, kuwaelimisha kwa kuwaweka karibu na vitalu, kutambua umuhimu wa upandaji, utunzaji na usimamizi wa mazingira.

Anaahidi kuendelea kupenda na kupanda miti kwa umoja, kwa sababu hata vijana zamani walipoharibu, shida kuu hawakuwa na uelewa sahihi, sasa wananuia 'darasa' la Agriwezesha, nao wataitumia kufanya makazi yao kuwaya kijani.

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (UN), usimamizi endelevu wa misitu ni muhimu mabadiliko ya tabianchi, pia kuhakikisha maisha bora ya baadaye.

Hivyo kutetea dhana hiyo, ndio maana kaulimbiu ya mwaka huu inahimiza; 'urejeshaji misitu; sauti ya kupona na ustawi'. Umoja wa Mataifa umetenga miongozo mmoja kati ya 2021 na 2030, mahususi wa ikolojia kurejesha misitu.

AFYA

# Wauguzi wakiri kuna 'vishoka' kati yao, waamua sasa kupambana nao

## • Dk. Mollel: Madaktari tusijione, bila wao hatuwezi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HADI sasa katika jamii, kunaelezwa kuwapo malalamiko ya wauguzi kutumika katika namna isiyo sahihi katika huduma yao kwa wagonjwa, hali inayoleta athari ya kiafya kwa wanaohudumiwa.

Shida kubwa inaelezwa ni kwa wauguzi na wakunga hao kushindwa kuzingatia maadili, wakijiegemeza katika vitendo viovu vya kujali maslahi yao, kuliko anachopaswa kutumikia mgonjwa.

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC), nalo katika hilo halijabaki kimya, limeamua kuchukua hatua dhidi ya malalamiko hayo, kwa kufuatilia kinachotokea ikichukua hatua dhidi ya watendaji mabaya, kadri inavyobidi.

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC), Agness Mtawa, anasema vitendo vya uvunjifu wa maadili, pamoja na kuwapo wauguzi na wakunga 'vishoka' wanaojiingiza katika taaluma hiyo, bado ni kikwazo cha tija katika sekta ya afya nchini.

Agness ameiambia hadhira iliyohudhuria mahafali ya saba, katika utoaji wa vyeti vya usajili na leseni kwa wauguzi na wakunga zaidi ya 1,000 waliofaulu kwenye mitihani ulioandaliwa na baraza hilo, jijini hapa.

"Pamoja na mafanikio tuliyoyapa, bado zipo changamoto mbalimbali, ikiwamo vitendo vya uvunjifu wa maadili kwa wauguzi na wakunga. Pia lipo tatizo la watu ambao siyo wanataaluma kuingilia taaluma yetu," anasema.

Hapo anasisitiza kwamba wauguzi na wakunga wanapaswa kuzingatia maadili, ili kuondoa malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza katika maeneo mbalimbali, ili kuisaidia serikali kupunguza vifo vya mama na mtoto.

"Sisi tutaendelea kuchukua hatua kwa muuguzi au mkunga yeyote ambaye atabainika kuwa amekiuka maadili kwa kumfuta kwenye usajili wetu," anatahadharisha.

### WALIOVUNJA MAADILI

Vilevile, anasema tangu mwaka 2016, wauguzi na wakunga 50 walibainika kuvunja maadili ya utumishi wa umma, kati yao wanne walifutiwa usajili na kupokonywa leseni, huku wengine wakipewa karipio kali.

Pia anataja kuwapo kero ya wauguzi na wakunga 'vishoka' wanaotumikia fani, akifafanua: "Bado wapo wananchi ambao wanajifanya wanataaluma hii na kutoa huduma bila ya kuwa na vigezo. Hili ni kosa la jinai!

"Ambao tumekuwa tukiwabaini tumewachukulia hatua za kuwapeleka mahakamani na wengine tayari wameshafungwa vifungo mbalimbali," anasisitiza Agness.

Kuhusu hatua za ziada kukabili hali hiyo, mkurugenzi huyo wa uuguzi anafafanua kwamba, hadi sasa baraza lao limeshaandaa mfumo wenye namna unaowawezesha waajiri wote kuhakiki usajili wa wauguzi na wakunga wote nchini.

"Mfumo huu unao uwezo wa kubaini muuguzi au mkunga aliyesajiliwa na asiyesajiliwa, hivyo nitoe wito kwa waajiri kufanya uhakiki kupitia mfumo huu mara kwa mara, ili kukabili changamoto ya wasio wanataaluma kujipenyeza," anasema.

Anataja hadi sasa kuna wauguzi na wakunga 55,000 waliosajiliwa nchini na wenye leseni hai wako 42,000, wakitoa huduma katika vituo mbalimbali vya serikali na binafsi.

Kiongozi huyo wa wauguzi anataja changamoto nyingine, ni wauguzi wengi kushindwa kuhuisha leseni zao kwa wakati kinyume na miongozi ya baraza hilo.

### MAMLAKA YA UUGUZI

Mkurugenzi wa Uuguzi na Ukunga Wizara ya Afya, Ziada Sellah, anawataka wauguzi na wakunga nchini kuacha tabia ya kuchagua maeneo ya kufanya kazi, akiwaasa wanapaswa kufahamu wahitaji wa huduma zao wako nchi nzima, hivyo hawana wasiishie kuchagua maeneo ya mijini pekee, kuwa pa kufanyia kazi.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Prof. Lilian Mselle anaahidi wataendelea kuchukua hatua kwa mtumishi yeyote atakayeoneka kuitia doa taaluma hiyo, kwa kuchangia uvunjifu wa maadili.

Prof. Mselle anasema: "Lengo la Baraza la Uuguzi na Ukunga kuanzishwa mwaka 1953 ilikuwa kusimamia maadili kwa kada hii, ili wananchi wapate huduma bora za afya."

Anasema, baraza hilo limeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kinidhamu kwa wauguzi na wakunga, ikiwamo kuwafutia leseni na kuwafuta kwenye daftari la usajili waliobainika kuwa na hatia.

### NAIBU WAZIRI AFYA

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, anasema katika mwaka wa fedha 2023, serikali imetenga Sh. bilioni nane kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kufanya kazi kwa wauguzi na wakunga nchini, Ikiwa ni pamoja na kuwasomesha kuwaongezea ujuzi.

Anasema, serikali inatambua umuhimu wa wauguzi na wakunga katika sekta ya afya, hivyo kuna haja ya kuwekwa mazingira mazuri ya ufanyaji kazi ili kuendelea kutoa huduma bora za afya katika maeneo mbalimbali.

"Takribani asilimia 60 ya watumishi waliopo katika sekta ya afya ni wauguzi na wakunga, hivyo hatuna budi kuweka mazingira mazuri kwa kuboresha mazingira ya kazi pamoja na kuboresha maslahi yao binafasi," anasema Dk. Mollel.

Rai yake kwa wauguzi na wakunga nchini ni kufanyika kazi kwa kuzingatia maadili, miongozo, kanuni na sheria, ili wamudu kutoa huduma bora kwa wananchi, hata kwa kupunguza malalamiko yaliyopo.

"Pamoja na kuboresha mazingira ya kazi, wauguzi na wakunga mnapaswa kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma, ili kuisadia serikali kutoa huduma bora na kupunguza vifo vya mama na mtoto," anaeleza.

Naibu Waziri Mollel, anawataka madaktari kufanya kazi kwa ushirikiano na watumishi wa kada ya uuguzi na ukunga, ili kuleta tija, hata kuifikia azma ya serikali kutoa huduma bora za afya kwa wananchi wake.

"Sisi madaktari tumekuwa watu wa kujiona ndiyo kila kitu, bila kujua kuwa bila wauguzi na wakunga hatuwezi, wauguzi wakikosea ndiyo sisi Wizara ya Afya, tutapiga hatua katika malengo tuliyojiwekea," anasema.



Wauguzi wakila kiapo cha maadili ya taaluma yao.



Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga, Agnes Mtawa (kushoto) na Mwenyekiti wa Baraza, Prof. Lilian Mselle, wakiwasha mshumaa kuashiria upendo kwa wagonjwa. **PICHA ZOTE: PAUL MABEJA**

> **"Ambao tumekuwa tukiwabaini tumewachukulia hatua za kuwapeleka mahakamani na wengine tayari wameshafungwa vifungo mbalimbali.**





# Mabula aonya kukithiri uvamizi maeneo ya wazi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameonya kukithiri kwa uvamizi wa maeneo ya wazi na umma na kuagiza wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kupima, kulinda na kusimamia maeneo hayo.

Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi 2022 zinaonesha kuwa miji inakua kwa asilimia 4.8 huku taarifa zikionesha kuna miji midogo inayochipukia 4,310 nchini ambayo isiposimamiwa ipasavyo itakuwa holela baadaye.

Dk. Mabula aliyasema hayo jana jijini hapo alipokuwa akifungua mkutano wa nane wa mwaka wa Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Mipango Miji.

Alisema wakurugenzi hao wanapaswa kulinda maeneo hayo ili kuondokana na mwenendo mbaya unaoendelea kukithiri wa kuvamia maeneo hayo.

"Umejitokeza utaratibu mbaya na usiovumilika wa kuvamia maeneo ya wazi, maeneo ya umma pamoja na maeneo hatarishi na kuyabadilisha kuwa ya matumizi mengine, hasa makazi, maeneo hatari kimazingira pamoja na maeneo ya wazi, yakiwamo maeneo maalum kwa matumizi ya baadaye yanapaswa kupimwa, kumilikishwa na kulindwa dhidi ya wavamizi," alisema.

Hata hivyo, alisema ili kuwe na miji nadhifu na iliyopangwa vyema katika nchi hawana budi kuanza kusimamia upangaji wa miji midogo na vitovu vya vijiji.

"Kwa kutambua umuhimu wa miji hiyo na uwapo wa kasi ndogo ya upangaji wa vijiji nchini, wizara imeandaa mwongozo wa upangaji na ujenzi wa nyumba bora vijijini ili kuwezesha jamii yetu kuanza kupanga maeneo yao kuanzia vijijini," alisema.

Aliagiza Bodi ya Usajili wataalam wa mipango miji na wanataaluma wote kuweka mkazo zaidi katika namna ya kuzuia miji midogo na vijiji kuwa makazi holela ya baadaye kwa kusimamia na kuelimisha jamii matumizi ya mwongozo wa upangaji na ujenzi wa nyumba bora vijijini.

Awali, alisema Sensa ya Watu na Makazi 2022 inaonesha kuna majengo 14,348.372 kati ya hayo asilimia 0.5 pekee ndiyo majengo ya ghorofa.

"Takwimu hizi zinaonyesha udhaifu mkubwa wa usimamizi wa sera na sheria tulizonazo ambazo zinaelekeza uendelezaji wa miji kwa ujenzi shadidi, natoa rai kwa Wakurugenzi wa Mamlaka za Miji, Manispaa na Majiji kupanga miji na kuifanya kuwa ya kiushindani kibiashara, kitalii na kimazingira ili iweze kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kuwa miji salama na mahali pazuri pa kuishi na kufanya kazi," alisema.

Aidha, alielekeza wataalamu wa mipango miji nchini kusimamia kikamilifu utekelezwaji wa mipango kabambe iliyoandaliwa katika maeneo yao na mipango kina ili kuwa na uendelezaji wa mji unaozingatia mipango miji.

"Ninyi wataalamu wa mipango miji mnapaswa kuwa na wivu na taaluma yenu na msiruhusu kuharibika kwa miji machoni mwenu," alisema.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Anthony Sanga, alisema sasa ni wakati wa kujikita kwenye TEHAMA ili kurahisisha wananchi kupata huduma kwa haraka na kuondokana na migogoro ya ardhi.

Awali, Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Mipango miji, Lucas Mwaisaka, alisema wataalamu wa mipango miji 508 wamesajiliwa huku kati yao 36 wamefutiwa usajili kwa kukiuka maadili ya taaluma hiyo.

Rais wa Chama cha Wataalamu wa Mipango miji Tanzania, Dk. Juma Matindana, aliomba kuharakishwa marekebisho ya muundo wa kada hiyo ili kuondokana na ukakasi uliopo.




Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Michael John (wa tatu kushoto), akikata utepe kuzindua Baraza la Pili la Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), mjini Singida hivi karibuni. Wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye (wa pili kushoto) na wajumbe wa baraza hilo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Shekhe apendekeza kuwekwa mabango kupinga ushoga

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHEKHE wa Mkoa wa Singida, Issa Nassoro, ametoa wito kwa Waislamu mkoani hapo kuandaa mabango yatakayokuwa na ujumbe wa kupinga vitendo vya mapenzi ya jinsia moja (ushoga) ambavyo vimeonekana kuanza kushamiri hapa nchini.

Nassoro alitoa wito huo jana wakati akizungumza katika kongamano la Jumuiya ya Vijana na Wanafunzi wa Kiislam (TAMSYA), Manispaa ya Singida katika maadhimisho ya Hijabu Day.

"Mmefanya jambo kubwa sana la suala la kuadhimisha Hijabu Day, lakini nitoe wito kwenu wa kuandaa mabango yenye ujumbe wa kupinga mapenzi ya jinsia moja ambapo wakati wowote kuanzia sasa tutatoa wito katika vyuo vyenu na shule zenu ili nasi tuweze kuonesha hisia zetu kwamba hatukubaliani na vitendo hivyo," alisema.

Shekhe Nassoro akizungumzia vazi la hijabu, alisema kuna baadhi ya watu wanalitumia vibaya kwa kuacha nyuso zao wanapokwenda kufanya uhalifu vikiwamo vitendo vya zinaa.

Alisema kupitia kongamano hilo kazi kubwa ni kutengeneza mioyo ya wanafunzi hao wa kike kuwa na hofu ya Mungu na kujikita zaidi katika imani ya Mwenyezi Mungu na ndipo lifuate suala la hijabu.

Katika hatua nyingine akizungumza katika kongamano la wanawake wa Kiislam aliwataka kujenga tabia ya kuwachunguza zaidi watoto wao wa kiume kutokana na kuwapo kwa vitendo vya kuingiliwa kinyume na maumbile kwa kuwa wao ndio walezi namba moja wa watoto hao.

Aliwaomba wanawake hao kuwa wabunifu na kufanya biashara ndogo ndogo zitakazowasaidia kupata kipato cha kujikimu na familia zao na kuwafanya watoto wao wa kike kutulia nyumbani na kuacha kujiingiza katika vitendo vya ukahaba ambavyo vimeshamiri katika maeneo kadhaa ya mjini hapa kwa kizingizio cha hali ngumu ya maisha.

Alisema Mufti wa Tanzania, Shekhe Abubakar Zubeiry Bin Ali, baada ya kuliona jambo hilo ameanzisha mfuko kwa ajii ya kuwasaidia wanawake wa kiislam na kutoa wito kwao kuanzisha vikundi na kwenda kukopa fedha hizo kwa ajili ya kuwasaidia na kuwataka kuwa waaminifu wa kurejesha mkopo huo.

Shekhe Nassoro alisema ni jambo la kushangaza kwa wanawake wa kiislam ambao Mungu amewapa afya njema, wanaona, wanamikono, wananguvu ya kufanya kila kitu, lakini wanashindwa kujiunga katika vikundi na kutafuta kipato halali badala yake wamekata tamaa ya maisha.

Aliwataka wanawake hao kwa kushirikiana na vyombo vya dola pamoja na viongozi wa kata wanakotoka kuhakikisha wanatokomeza madanguro yote ya ukahaba kwa kuwa hayakubaliki na nchini hakuna leseni ya vitendo hivyo.

## Serikali yabaini ongezeko vitendo vya ukatili kijinsia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imebaini kuwa ongezeko la matukio ya ukatili wa kijinsia kwa asilimia 4.1 kwa mwaka 2022.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis, alibainisha hayo jana alipokuwa akifungua Mkutano wa Wadau wa Ustawi wa Jamii uliofanyika jijini hapo.

Alisema kwa mujibu wa taarifa kutoka Jeshi la Polisi ya mwaka 2022, jumla ya matukio 30,566 yameripotiwa kati ya hayo watu wazima 18,403 na watoto 12,163 ikilinganisha na 29,373 yaliyoripotiwa 2021 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 4.1.

Pia alisema vitendo vya ukatili dhidi ya watoto bado ni tatizo katika jamii kutokana na kuongezeka hapa nchini na kwa asilimia kubwa vinafanywa na ndugu au watu wa karibu.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau itaendelea na jitihada za kupambana na mila na desturi potofu zinazochochea ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na wanawake.

"Vitendo hivi vinaathiri ukuaji wa watoto na vinasababisha nguvu kazi dhaifu isiyokuwa na tija ya kutosha katika taifa kwa siku za usoni. Hivyo ni jukumu letu sote kulinda haki na ustawi wa mtoto kwa kuelimisha wazazi/walezi na jamii kwa ujumla ili kuboresha huduma ya mlezi chanya kwa watoto," alisema.

Aliwaasa wadau wa huduma za ustawi wa jamii kuchangia utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mfumo wa ustawi wa jamii nchini unaoitwa mfumo jumuishi ili kusaidia kuwezesha upatikanaji wa watoa huduma usu za ustawi wa jamii.

Naye Ofisa Tawala Mkuu kutoka Wizara hiyo, Jonathan Kyando, akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. John Jingu alisema serikali inatambua jitihada zinazofanywa na wadau wa huduma za ustawi wa jamii.

Kyando aliwahimiza wadau hao kuboresha uratibu na utoaji wa huduma stahiki kwa makundi yote yanayopatiwa huduma za ustawi jamii.



# Mbaroni tuhuma kuingiza vipodozi vyenye sumu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIJANA wawili ambao ni dereva na utingo wa lori la mafuta, wanashikiliwa na Polisi kwa tuhuma za kuingiza nchini shehena ya vipodozi vyenye viambata vya sumu na vilivyopigwa marufuku kwa kutumia roli walilokuwa wakiliendesha.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, aliwataja ni Fahmi Ahmed (33) mkazi wa Kigamboni jijini Dar es Salaam na Mohamed Mawazo (26) mkazi wa Mabibo pia jijini Dar es Salaam.

Alisema vijana hao walikamatwa wakisafirisha maboksi 1,052 ya vipodozi hivyo kwa kutumia lori Axon Benz lenye namba za usajili T.900 DEV na tela namba T.800 DEL ambalo linamilikiwa na moja ya kampuni ya usafirishaji.

Kamanda Kuzaga alisema watuhumiwa walikamatwa juzi saa 3:30 asubuhi katika Kijiji cha Songwe baada ya kuvuka Mkoa wa Songwe na kuingia Mbeya.

Alisema walikamatwa na makachero wa jeshi hilo waliokuwa wameweka mtego katika eneo hilo la Songwe baada ya kupata taarifa za siri kutoka kwa raia wema na walipopekua gari hilo walibaini kuwa vijana hao walikuwa wamebeba mzigo ambao haujulikani.

Alisema walipopekuwa kwenye vyumba vya kubeba mafuta walibaini kuwa kulikuwa na makasha hayo ambayo yana aina 13 tofauti za vipodozi hivyo vyenye viambata vya sumu.

Alizitaja aina ya vipodozi vilivyokamatwa kuwa ni Epiderm boksi 38, Coco pulp boksi 159, Citro light boksi 87, Carolight boksi 152, Prety white boksi 22, Coco pulp maji boksi 100, Gluta white boksi 59, Diproson boksi 41, Pawpaw boksi 91, Extra clair boksi 50, Clear therapy Ct + boksi 164, Betason boksi 72 na Nacitro light boksi 87.

Alisema vijana hao walikuwa wanasafirisha mzigo huo kutoka nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na mpaka sasa bado mmiliki halali wa mzigo hajulikani huku vijana hao wakiendelea kuhojiwa.

"Tulipowahoji walikiri lakini tulipowataka nyaraka walikuwa hawana hata moja na ndipo tulipowasiliana na wenzetu wa Mamlaka ya Mapato (TRA) na Shirika la Viwango nchini (TBS) ili kubaini kama mzigo huu ni halali," alisema Kamanda Kuzaga.

Aliwataka wananchi kuacha kufanya biashara hizo za magendo kwa maelezo kwa jeshi hilo linaendelea kubuni mbinu mbalimbali za kubaini na kudhibiti mizigo yote ya magendo. Meneja wa TRA Mkoa wa Mbeya, Musibu Shaban, alisema mpaka sasa thamani halisi ya mzigo huo haijafahamika, wanaendelea kufanya hesabu za kiforodha ili kubaini kiasi cha fedha ambacho serikali ingepoteza endapo mzigo huo ungeingia sokoni.

Alisema uingizaji wa bidhaa za magendo nchini unakiuka Sheria ya Forodha ya Afrika Mashairiki, wataendelea kulishikilia gari lililotumika pamoja na watuhumiwa hao wakati hatua za kisheria zikiandaliwa.

"Kifungu namba 199 na 200 vya Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 inasema pamoja na kushikiliwa mtu anayesafirisha bidhaa za magendo lakini pia chombo kinachotumika kinatakiwa kushikiliwa pia kwa hiyo hili gari tutaendelea kulishikilia kwa ajili ya hatua zaidi," alisema Shabani.



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, ACP Benjamin Kuzaga (aliyevaa glovu), akionyesha sehemu ya makasha 1,052 yenye vipodozi vyenye viambata vya sumu baada ya kuwakamata vijana wawili wakisafirisha kwa kutumia lori la mafuta, kwa kushirikiana na maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) mkoani humo juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Waliovamia vyanzo vya maji watakiwa kuondolewa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imewaagiza wakuu wa wilaya kushirikiana na taasisi mbalimbali kuwaondoa wananchi wote waliovamia vyanzo vya maji ili kuhakikisha vyanzo hivyo vinakuwa endelevu.

Pia kuwaondoa wavamizi wa misitu ambao wanafanya shughuli mbalimbali za kibinadamu ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayoikabili dunia miaka ya karibuni.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa agizo hilo jana wakati wa uzinduzi wa upandaji miti katika Ofisi za Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema uharibifu wa vyanzo vya maji unasababisha kupungua kwa maji kwa ajili ya matumizi ya shughuli mbalimbali ikiwamo uzalishaji wa nishati ya umeme, shughuli za kilimo pamoja na matumizi ya nyumbani.

"Msiogope kuwaondoa kwa sababu wale wanakuwa wamevunja sheria za nchi, maji yakikosekana hao ndio huwa wanakuwa wa kwanza kulalamika na wakati mwingine wanatusemea kwa viongozi wa juu," alisema Homera.

Alisema miti inayopandwa inatakiwa kutunzwa ili istawi na isaidie kupunguza tatizo la mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuhakikisha mazingira yanakuwa rafiki kwa maisha ya binadamu.

# TBS yatakiwa kusaidia wajasiriamali ubora bidhaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKA la Viwango nchini (TBS) limetakiwa kuwasaidia wajasiriamali wadogo kuzalisha bidhaa zenye ubora kwa kutoa elimu kuhusu viwango vya ubora pamoja na kuwatembelea mara kwa mara kwenye maeneo yao ya uzalishaji ili wazalishe bidhaa zinazokidhi viwango vya kisheria.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa anafunga maadhimisho ya Siku ya Viwango barani Afrika ambayo kitaifa yalifanyika jijini Mbeya na kushirikisha makundi mbalimbali ya wananchi.

Malisa alisema kwenye jamii kuna bidhaa ambazo zinazalishwa na kusambazwa kwa wananchi bila kuthibitishwa ubora wake kutokana na baadhi ya wazalishaji kutojua na baadhi yao kukwepa kwenda kwenye ofisi za TBS.

Vilevile, alisema ili kudhibiti viwanda bubu ambavyo vinazalisha bidhaa mbalimbali, shirika hilo linatakiwa kuhakikisha linakuwa na maofisa kwenye wilaya zote nchini ili wawe wanafuatilia na kudhibiti uzalishaji wa bidhaa hizo.

"Nashauri maofisa wa TBS msikae ofisini, nendeni kwa wananchi wanakozalisha bidhaa ili kama wanazalisha zisizokidhi viwango muwe askari wa kwanza kung'ata, huko mitaani kuna baadhi ya bidhaa zinazalishwa na viwanda bubu zikiwamo pombe," alisema Malisa.

Alisema shirika hilo linatakiwa kuhakikisha linashirikiana na taasisi zingine likiwamo Jeshi la Polisi katika kudhibiti bidhaa feki ili kuokoa maisha ya wananchi wanaozitumia.

Mkurugenzi wa TBS, David Ndibalema, alisema maadhimisho ya siku ya viwango barani Afrika huwa yanafanyika Oktoba 14 kila mwaka lakini Tanzania inaadhimisha mwezi machi kwa sababu oktoba 14 huwa ni siku ya mapumziko ambayo Watanzania huwa wanaadhimisha kifo cha Hayati baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere.

Alisema maadhimisho hayo yalifanyika kwa siku mbili katika Mkoa wa Mbeya kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wananchi wa kawaida, wakulima, wajasiriamali wanaozalisha na kuuza bidhaa mbalimbali.

Pia walianza kwa kutoa mafunzo maalumu kwa makundi yaliyoshiriki ili kuyawezesha kutambua taratibu za ubora ili wazalishe bidhaa ambazo zinakidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

Maadhimisho hayo yaliambatana pia na mashindano ya uandishi wa insha kwa wanafunzi wa vyuo vikuu mbalimbali nchini kwa lengo la kuendelea kukuza uelewa wa wananchi kuhusu viwango.

"Washindi wetu watatu wa uandishi wa insha watatuwakilisha taifa letu kwenye shindano hilo katika Bara la Afrika, mashindano haya yalianza mwaka 2014 yalipoanzishwa maadhimisho haya, mwaka jana mmoja wa wawakilishi wetu alishika nafasi ya tatu kwa hiyo na mwaka huu tunaamini watatuwakilisha vizuri," alisema Ndibalema.

Baadhi ya washiriki katika shindano la tuzo na kushinda, waliahidi kwenda kuliwakilisha vizuri taifa kwenye mashindano ya Afrika ambayo yatafanyika mwezi Oktoba.

Mmoja wa washiriki hao, Justa Desdery ambaye ni msichana pekee aliyeingia kwenye 10 bora alisema shindano hilo ni muhimu kutokana na kuwasaidia wanafunzi na wadau kujua vitu vingi kuhusu ubora.



# Tunzo ya Taifa ya Mwl. Nyerere kukutanisha waandishi bunifu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUNZO ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya uandishi bunifu inatarajiwa kufanyika Aprili 13, mwaka huu, jijini Dar es Salaam ambayo itawakautanisha waandishi bunifu wa vitabu, riwaya, hadithi na mashairi wa ndani na nje ya nchi.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda, alisema tunzo hizo ni kwa ajili ya uandishi wa riwaya, hadithi fupi, mashairi, vitabu vya watoto, tamthilia na wanaofanya tafsiri ya vitabu vingine kutafsiri kwa Kiswahili ili kukuza uandishi bunifu wa lugha hiyo.

Aliyasema hayo jana mjini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tunzo hiyo.

Alisema shindano hilo litasaidia kukuza usomaji ili wananchi waendeleze elimu, kujiamini, kuwasiliana na dunia na kuimarisha sekta ya uchapishaji wa vitabu ambalo inapita katika kipindi kigumu kwa sababu ya kukosa soko.

Alisema kazi ya uandishi bunifu inasaidia kuhifadhi na kueneza utamaduni na kutoa mfano wa mwandishi Abdulrazaki Muna ambaye vitabu vyake vinaonesha mandhari ya Zanzibar.

"Tukiwa na waandishi bunifu wengi wanaoandika vizuri yana uwezo wa kushinda katika tunzo ya kimataifa," alisema.

Prof. Mkenda alisema ingependeza mbele ya safari kuwa na waandishi bunifu wa Tanzania ambao uandishi wao utakuwa maarufu duniani na kutafsiriwa katika lugha mbalimbali.

Alisema katika tunzo hizo mshindi wa kwanza atapata kitita cha Shilingi milioni 10, wa pili milioni saba, wa tatu milioni tano na mshindi wa nne hadi 10 watapatiwa vyeti vya kutambuliwa kushiriki mashindano hayo.

Mwenyekiti wa kamati ya tunzo hiyo, Prof. Penina Mlama, alisema tunzo hiyo imepokelewa kwa hamasa kubwa kwa kuwasilishwa kazi 283 kati ya hizo 193 ni mashairi na 83 riwaya.

Alisema majaji wamejifungia wakiendelea kusoma na kuchataka kazi hizo na washindi watatambulika.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulgulam Hussein, alisema tunzo hiyo inafanywa kwa ushirikiano wa wizara zote mbili ya SMZ na SMT katika kuimarisha Muungano. Alisema tunzo hiyo ni muhimu kwa sababu Mwalimu Nyerere ana mchango mkubwa Afrika na duniani na itasaidia kukuza lugha ya Kiswahili.

Tunzo hiyo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya uandishi bunifu itakuwa endelevu na kwa mwaka huu Wizara ya Elimu imetenga Shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya maandalizi ya tunzo hiyo na fedha za washindi zinatokana na bajeti hiyo.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Zanzibar jana, kuhusu tuzo ya Mwalimu Nyerere ya uandishi bunifu inayotarajiwa kufanyika Aprili 13, mwaka huu, jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Carolyne Nombo na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulgulam Hussein. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZEC yatangaza uchaguzi mdogo Mtambwe

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi Zanzibar imetangaza uchaguzi mdogo wa Jimbo la Mtambwe, Pemba baada ya aliyekuwa mwakilishi wa jimbo hilo, Habib Ali Mohammed kufariki dunia.

Kwa mujibu wa ZEC, uchaguzi huo utafanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji mstaafu Hamid Mahmoud, alisema uchaguzi mdogo hutakiwa kufanyika endapo mjumbe aliyechaguliwa katika uchaguzi mkuu atafariki dunia, atajiuzulu au atapoteza uanachama wa chama alichogombea nafasi aliyokuwa nayo na kusababisha kupoteza sifa yake.

Alisema Machi 6, mwaka huu, Tume ya Uchaguzi Zanzibar ilipokea taarifa kutoka kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi kuwapo wazi kiti cha Baraza la Wawakilishi kutokana na kifo cha aliyekuwa mwakilishi wa jimbo hilo kilichotokea Machi 3, mwaka huu.

Kutokana na taarifa hiyo Tume inawajibika kisheria kuendesha uchaguzi mdogo wa jimbo hilo ili kujaza nafasi aliyekuwa mwakilishi wa jimbo hilo kama inavyoeleza Sheria ya Tume hiyo kifungu 40(2) na (3) cha Sheria ya Uchaguzi namba 4 mwaka 2018.

Aidha, alisema kwa kuzingatia maelekezo ya Sheria ya Uchaguzi, Tume ina wajibu wa kutekeleza kwanza kutangaza tarehe ya uteuzi kwa ajili ya uchaguzi huo ndani ya siku 30 tokea kifo cha mjumbe wa Baraza la Wawakilishi chini ya miezi minne na sio zaidi ya miezi 12 toka kiti kuwa wazi.

Alisema Tume imejipanga kuhakikisha kuwa uchaguzi huo mdogo unafanyika bila ya uvunjaji wa sheria za uchaguzi.

Pia Oktoba 1 hadi 7 uchukuaji na urejeshaji wa fomu za mgombea utaanza na Oktoba 8, wagombea watateuliwa na Oktoba 11 ni siku ya kampeni ambazo zitafungwa Oktoba 26.

Mwenyekiti huyo alisema wapigakura watakaotumika katika uchaguzi huo mdogo ni waliomo katika daftari la wapigakura la awali na Tume haina mpango wa kuwaandikisha wapigakura wapya.

Aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kufuatilia mchakato huo ili ufanyike kwa mujibu wa sheria za tume na kufanya uchaguzi kuwa huru na wa haki.

## Wakala wa uwezeshaji wasaidia wananchi kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema maendeleo makubwa yamepatikana kupitia uwakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na ukuaji wa uchumi umeimarika zaidi na kuchangia kipato kwa wananchi.

Akizungumza jana huko katika kituo cha asali Kizimbani Unguja, wakati akifungua mafunzo ya upatikanaji wa sumu ya nyuki pamoja na jeli ambayo ina thamani kubwa kwa maendeleo ya wajasiriamali na taifa kwa ujumla.

Alisema dhamira ya serikali ni kuwawezesha wajasiriamali na kuwaandalia mazingira rafiki ambayo yatawawezesha kupata elimu, mikopo na mitaji ili kuendeleza bidhaa zao.

Alisema serikali kupitia taasisi ya uwakala uwezeshaji wananchi kiuchumi imewekeza fedha nyingi kwa lengo la kuwasaidia wajasiriamali na hasa wadogo pamoja na kuwaandalia mazingira mazuri ambayo yatawawezesha kuendesha shughuli zao. Alisema kuwa shughuli za ujasiriamali kwa wakati huu zimechukua idadi kubwa ndani ya jamii mjini na vijijini kuwasaidia kupata kipato chao kutokana na kazi za ujasiriamali.

Mkufunzi wa mafunzo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kijiji cha Nyuki kilichopo Singida, aliitaka jamii kuhamasika zaidi na kujishughulisha na kazi za ujasiriamali hasa katika ufugaji wa nyuki ambao ndani yake kuna mazao yenye faida kubwa zaidi kwa maisha ya binadamu. "Kuna idadi kubwa ya mazao yanayotokana na zao la nyuki ambayo yanafaida kubwa kwa watumiaji hivyo ni vyema jamii kuhamasika na kuzichangamkia fursa zilizopo zinazotokana na mazao ya nyuki kwa faia yao na taifa kwa ujumla," alisema.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo waliitaka serikali kuendelea kuwapa ushirikiano zaidi pamoja na kuundwa kwa sera na sheria ambazo zitawalinda na kuwawezesha kuendeleza kazi zao kwa ufanisi zaidi.

MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**ABRAHAMAN SWALEHE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0485-0221 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MAJENGO SEKONDARI** mwaka 2015. Cheti cha Chuo **(WATER QUALITY LABORATORY TECHNOLOGY)** chenye namba **OD/2017/WL151** kilichotolewa na **WATER INSTITUTE** mwaka 2020. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za polisi: **DAR/CHU/RB/9384/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NASSER ADAM KINGU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 130 DJN – BREVIS.** Chassis No. **JCG100056043.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/410283/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya BAGAMOYO**
**Kituo cha KISARAWE Mkoa PWANI**
**Shauri la Madai Ndoa Na. 15/2023**
**Jina la mdai: JOHN TITO SALEHE**
**Jina la Mdaiwa: EVA ALLY KAMATA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa: EVA ALLY KAMATA**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba**

### KUJA KUJIBU MADAI YA TALAKA

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 03 Mwezi wa 04 Mwaka 2023 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 27 Mwezi wa 03 Mwaka 2023.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**
**MATRIMONIAL CAUSE NO. 5/2023**
**ELISEI MLABU CHILALA ....APPLICANT/PETITIONER.**
**VERSUS**
**AGRIPINA WILLIAM MZENGA ......RESPONDENT**
**TO: AGRIPINA WILLIAM MZENGA**

### NOTICE OF DATE OF MENTION /HEARING

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for hearing/Mention on 18 day of 04, 2023 at 9:00 am.

Before Hon N. J. Tungaraja RM/SRM

YOUR ARE required to appear in this court on the fixed date without fail and you may bring with you all required documents in support of your case.

Given under my hand and the seal of the Court this 28 day of MARCH,2023

COURT SEAL
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI NA. 256 YA MWAKA 2022**
**AESHI GEORGE MAZENGO ............................MDAI**
**VERSUS**
**EMILIA MAKOCHO ..................................MDAIWA 1**
**EMILIA CHITETO ...................................... MDAIWA 2**
**MKUNDA MANYIKA ................................ MDAIWA 3**

**KWA:**
**MKUNDA MANYIKA**
**POPOTE ULIPO.**

### YAH: KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 03.05. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 29 ya mwezi wa MACHI, 2023.

MWENYEKITI

## NOTISI/ TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART & GENERAL BROKERS** kwa mamlaka tuliyopewa na **VICTORIA FINANCE PLC, AKIBA COMMERCIAL BANK PLC , BRAC na NMB BANK** kwa mujibu wa sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,tunatoa notisi ya kulipa madeni kwenye taasisi zote nne kwa mdaiwa hapo chini ndani ya siku 7 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya mnada wa marudio wa hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| s/No. | Jina la Mdaiwa | Jina la mdhamini | Dhamana | Mahali ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | ROSEMARY ALOYCE MOSHA | ROSEMARY ALOYCE MOSHA | Nyumba | KIMARA TEMBONI MTAA WA MJIMPYA-UBUNGO | 06/04/2023 Kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0788411524/0714939933.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HAMIS ISAACK JACOB** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA **SUZUKI CARRY** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 354 CSD.**KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI: TAARIFA YA POLISI **KAH/TR /RB/220/2023.**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA SONGEA.**
**MAHALI.................SONGEA**
**MAOMBI NO 40, 2022**
**BENO .B. NYONI ................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**RAJESHI WILLIAM ........... MJIBU MAOMBI**

### WITO /KUITWA SHAURINI

**KWA –RAJESHI WILLIAM**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kusikilizwa hukumu tarehe 31 Mwezi 03 mwaka 2023 saa 2:00 Asubuhi mbele ya mheshimiwa 1.J.AYO Mwenyekiti wa Baraza .Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza hili leo tarehe **24 Mwezi 03 mwaka 2023.**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
SONGEA

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 430 LA 2017**
**HAPPYNESS ROMAN....... MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**JOSEPHAT MALIMA.......MDAIWA/WADAIWA**

### WITO KUITWA SHAURINI

**JOSEPHAT MALIMA**
**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**HAPPYNESS ROMANI** Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe **30/3/2023 Saa TATU (3:00)** Asubuhi mbele ya **Mh. J. W. SILLAS** Hivyo unaarifiwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe **27 Mwezi 03 Mwaka 2023**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ZUBERI HASSANI ZUBERI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 571 AKM**. Chassis No. **27129301** Engine No. **54931293.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi au piga simu namba **+255655023127.** Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/113383/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPKI

**MBUGANI MBUGANI FELECIAN** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC.494 DBT.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KWA RB NAMBA **MWA/NY/RB/112130/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MKUYUNI**
**WILAYA YA NYAMAGANA**
**SHAURI LA MADAI YA PESA NAMBA 44 YA MWAKA 2023**
**BHOKE SARIRO..........MDAI**
**DHIDI YA**
**SYLVESTER MLOKOZI......MDAIWA**
**KUITWA SHAURINI**
**KWA : SYLVESTER MLOKOZI**

### POPOTE ULIPO

MAHAKAMA HII INAKUFAHAMISHA KWAMBA MDAI AMEFUNGUA MADAI DHIDI YAKO.

SHAURI LIMEPANGWA KUSIKILIZWA MNAMO TAREHE 06/04/2023 SAA 2:30 ASUBUHI KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MKUYUNI NA UNATAKIWA KUWEPO, AU KUWAKILISHWA KISHERIA PAMOJA NA KULETA UTETEZI WAKO DHIDI YA MAOMBI HAYA.

ZINGATIA KWAMBA KUTOKUFIKA KWAKO TAREHE HIYO, SHAURI LITAANZA KUSIKLIZWA BILA WEWE KUTAARIFIWA TENA, NA MAAMUZI KUTOLEWA.

IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA MHURI WA MAHAKAMA HII LEO 23/03/2023

M.L KILENZI
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO MKUYUNI
MWANZA

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701

OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

MOB: +255 - 0677020701

E-mail: advertise@guardian.co.tz,

Website: www.ippmedia.com

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Odinga amshutumu Ruto kwa uchochezi

**NAIROBI,** Kenya

KIONGOZI wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga, ameituhumu serikali ya nchi hiyo kuchochea vita kwa msingi wa matabaka.

Raila Odinga (pichani) ametoa matamshi hayo kufuatia uvamizi wa genge la wahalifu katika shamba linalomilikiwa na familia ya rais wa zamani, Uhuru Kenyatta, Jumatatu ya wiki hii. Kiwanda cha gesi kinachomilikiwa na familia ya Odinga pia kilishambuliwa siku hiyo, na watu wanaoshukiwa kuwa wafuasi wa Rais William Ruto, kama ulipizaji kisasi kwa maandamano ya upinzani dhidi ya serikali.



Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari uliorushwa moja kwa moja katika kituo cha televisheni cha K24, chenye mafungamano na familia ya Kenyatta, Odinga alidai kuwa walichokitabiri wakati wa kampeni kuwa kambi ya Ruto ilikuwa ikiandaa vita vya kimataba kimedhihirika.

Alionya kuwa huo ni mwanzo wa kusambaratika kwa serikali ya Ruto.

Licha ya mashambulizi hayo yaliyozilenga mali za familia yake na ya Kenyatta, Raila Odinga aliapa kuwa maandamano yataendelea kila Jumatatu na Alhamisi. **DW**

# Afukuzwa Indonesia kwa kunajisi mlima

**BALI,** Indonesia

MWANAMUME mmoja raia wa Russia, atafukuzwa nchini Indonesia baada ya kuvua nguo zake akiwa katika kisiwa cha Bali, ambao unaaminika na wenyeji kuwa mtakatifu.

Picha ya mwanamume huyo akiwa ameweka suruali yake kwenye vifundo vyake vya miguu juu ya mlima Agung, ilisambaa mitandaoni wiki iliyopita.

Mwanamume huyo aliyetambulika kwa jina moja la Yuri, ameomba msamaha lakini atazuiwa kuingia tena nchini humo kwa miezi sita.

**Kitendo changu hakina kisingizio. Kitu pekee kilichosababisha kilichotokea ni ujinga wangu binafsi.**

Hivi karibuni Bali imeongeza juhudi za kukabiliana na watalii wa kigeni wanaotajwa kukosa maadili.

Mlima Agung, sehemu ya juu zaidi katika kisiwa hicho, inaaminika na Wahindu kuwa makao ya miungu.

"Alikiuka kanuni na hakuonyesha heshima kwa utamaduni wetu," alisema Mkuu wa Ofisi ya Sheria na Haki za Kibinadamu ya Bali, Anggiat Napitupulu.

Katika video iliyowekwa kwenye Instagram kwa lugha ya Kirussia, Yuri alisikika akiomba msamaha "Kitendo changu hakina kisingizio. Kitu pekee kilichosababisha kilichotokea ni ujinga wangu binafsi."

Baadaye alishiriki katika hafla maalum ya utakaso wa mlima huo, tambiko ambalo mara nyingi hufanyika na wenyeji baada ya matukio kama haya.

Wijaya, balozi mdogo wa heshima wa Russia huko Bali, aliiambia CNN Indonesia, kwamba mtalii huyo alikuwa na wazimu na kwamba kumfukuza ni jambo sahihi la kufanya. Wenyeji wengi kwenye mitandao ya kijamii pia waliunga mkono kufukuzwa kwake. **BBC**




Mwandamanaji akishikilia msalaba wenye neno 'amani', wakati wa maandamano ya kupinga mageuzi ya pensheni ya serikali, Paris nchini Ufaransa juzi. **PICHA: EPA-EFE**

# Serikali yakanusha kutaka kumuua rais mstaafu

**GABORONE,** Botswana

SERIKALI ya Botswana imepuuza madai kwamba inapanga kumkamata na kumuua rais wa zamani ambaye anaishi uhamishoni, Ian Khama, iwapo atarejea nchini mwake.

Katika mahojiano wiki iliyopita, Khama aliliambia shirika la habari la AFP kwamba alikuwa na taarifa kuhusu mipango ya kumkamata na kumpa sumu mara atakapofika nyumbani kwake atakapotoka Afrika Kusini, ambako anaishi tangu 2021.

Alidai serikali ya Botswana inahofia ushawishi wake kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka ujao.

Lakini katika taarifa yake ya juzi, katibu mkuu wa mawasiliano William Sentshebeng, alipuuza madai hayo akisema ni ya kukasirisha na ya kusikitisha.

"Tunayachukulia madai hayo kuwa yamechochewa kisiasa na kwa nia moja tu ya kuchafua sifa nzuri ya Botswana na serikali yake," alisema Sentshebeng.

Huku uchaguzi ukikaribia mwaka ujao, Khama ameapa kumng'oa mrithi wake Mokgweetsi Masisi, ambaye sasa ni mpinzani mkubwa anayemtuhumu kuwa tishio kwa demokrasia.

Khama alisema anajiandaa kurejea nyumbani kujiunga na vyama vingine ili kuhakikisha kwamba Masisi na chama chake wanashindwa katika uchaguzi.

Kiongozi huyo wa zamani alisema amefanyiwa uchunguzi kamili wa matibabu na kusafisha wosia wake kwa sababu alikuwa na uhakika kwamba ndani ya siku chache baada ya kuwasili atakamatwa.

Khama mwenye umri wa miaka 70, ofisa mkuu wa zamani wa kijeshi, alitawala tiafa hilo tajiri barani Afrika kwa kuzalisha almasi kwa wingi.

Mzozo kati yake na mrithi wake ulianza 2018 wakati Rais Masisi, alipoanza kubadili baadhi ya sera kuu zilizopitishwa wakati wa uongozi wa Khama.

Mnamo Januari, Rais Masisi alitia saini makubaliano ya maridhiano lakini ushindani kati ya wawili hao unaendelea.

Mnamo Desemba mwaka jana, Botswana ilitoa hati ya kukamatwa kwa Khama, kwa madai ya kumiliki silaha kinyume cha sheria.**BBC**

# Spika Ghana amkosoa Kamala

**ACCRA,** Ghana

SPIKA wa Bunge nchini Ghana, amekosoa matamshi ya Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, ambaye alihimiza kuhusu haki za wapenzi wa jinsia moja (LGBTQ) wakati akiwa nchini humo.

Wabunge wa Ghana wanajadili mswada wa Kukuza Haki Sahihi za Kijinsia za Kibinadamu na mswada wa Thamani ya Familia ya Ghana, ambayo inaharamisha utetezi wa haki za wapenzi wa jinsia moja na kupendekeza adhabu ya vifungo jela kwa wale wanaojitambulisha. Spika Alban Bagbin, aliwataka wabunge kutotishwa na mtu yeyote.

"Demokrasia ni nini? Kwamba lazima mtu aniandikie lipi jema na lipi baya? Sijasikika, kwani tumeamua kujishusha thamani na kwenda kuombaomba?" alisema.

Harris hakuwa ameshughulikia mswada huo moja kwa moja wakati wa kikao chake na Rais Nana Akufo-Addo siku ya Jumatatu, lakini alisema ni suala ambalo analichukulia kuwa suala la haki za binadamu na ambalo halitabadilika.

Spika Bagbin aliwaambia wabunge kwamba mswada huo unazingatia katiba na utapitishwa. Alimuonya Rais Akufo-Addo dhidi ya kuingilia kati suala hilo.

"Hili ni neno kwa rais hakuna jinsi anaweza kuingilia kati, subiri hadi tupitishe, ndipo uapoingia," aliwaambia wabunge huku kukiwa na shangwe na makofi.

Mapenzi ya jinsia moja tayari yana adhabu ya kifungo cha hadi miaka mitatu jela nchini Ghana, ambapo mitazamo ya chuki imeenea na kusababisha rasimu ya sheria hiyo kupendekeza adhabu kubwa. **BBC**

# AZAM FC YAANZA HESABU KUIKARIBISHA MTIBWA FA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kumalizika kwa kalenda ya kimataifa, kikosi cha Azam FC kinatarajia kuingia kambini leo kuanza maandalizi ya mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA (ASFC), dhidi ya Mtibwa Sugar kutoka Turiani, Morogoro, imeelezwa.

**Azam FC watakuwa nyumbani kuwaalika Mtibwa Sugar mchezo utakaochezwa Jumatatu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Kalimangonga Ongala 'Kally', alisema kikosi chake kimeingia kambini ili kujiimarisha na kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na kusonga mbele katika michuano hiyo.

Kally alisema mechi ya kirafiki waliocheza dhidi ya KMC FC imewasaidia kutatua mapungufu yao ikiwamo safu ya ushambuliaji ambayo imetumia vyema nafasi wanazotengeneza na kupata mabao mengi.

"Tumeona mabadiliko madogo baada ya kucheza na KMC FC, tumecheza mpira mzuri hasa safu ya ushambuliaji kwa kuwa makini katika kutumia vizuri nafasi tulizozitengeneza na imani kubwa ya mechi ijayo tutafanya vizuri," alisema Kally.

Kocha huyo alisema anawafahamu vizuri wapinzani wao kwa sababu ya ubora walioufanya wa kuboresha kikosi katika kipindi cha dirisha dogo, hivyo wanatarajia kuongeza umakini katika mchezo huo.

"Tunahitaji ushindi ili tusonge mbele ikiwezekana kutwaa ubingwa kwa Kombe la Shirikisho (FA), kwa sababu tumeshindwa kupambana katika kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara, sasa hatutaki kurejea makosa," alisema kocha huyo.

Bingwa wa mashindano hayo hupata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma (wa pili kushoto) na Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali wa benki ya NBC, James Meitaron (wa pili kulia), wakimkabidhi kombe mshindi wa mashindano ya NBC Lugalo Open 2023, Ally Mcharo wa klabu ya TPC, Kilimanjaro katika hafla iliyofanyika kwenye viwanja vya Jeshi vya Gofu Lugalo, Dar es Salaam hivi karibuni. Kushoto ni Mwenyekiti wa Klabu ya Lugalo, Brigedia Jenerali Mstaafu, Michael Luwongo na Rais wa TLGU, Queen Siraki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Kikapu walemavu kuchuana Dar*

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Mpira wa Kikapu kwa Watu wenye Ulemavu (TWBA), kimesema mechi ya mtoano ya Timu ya Taifa ya Wanawake dhidi ya Kenya iliyopangwa kuchezwa Nairobi, sasa itafanyika Mei 5 hadi 7, mwaka huu jijini, Dar es Salaam, imefahamika.

Mshindi wa mechi hiyo atapata tiketi ya kushiriki mashindano ya Paralimpiki Afrika yatakayofanyika Agosti, mwaka huu nchini Ghana.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa TWBA, Abdallah Mpogole, alisema Kenya imeshindwa kuandaa na Shirikisho la Kimataifa la mchezo huo (IWBF) likalazimika kuuhamishia hapa nchini.

Mpogole alisema anaiomba serikali na wadau mbalimbali kuwasaidia fedha kwa ajili ya maandalizi pamoja na kununua vifaa vya michezo.

Naye Kocha Mkuu wa Timu ya Tanzania, Khadija Karambo, alisema timu yake inaendelea vyema na mazoezi kwenye viwanja vya JMK Park.

"Tumejiandaa vizuri kuhakikisha ndoto zetu za kupata nafasi ya kwenda Ghana kushiriki mashindano ya Paralimpiki Afrika zinatimia," alisema Karambo.

Wakati huo huo, Timu ya kikapu ya walemavu ya wanaume ambayo imefuzu kushiriki Mashindano ya Paralimpiki Afrika inatarajia kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Kenya itakayofanyika Mei 5, mwaka huu.



## Singida Big Stars yaliota taji la FA

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Singida Big Stars kimeweka kambi yake jijini Dodoma kwa ajili ya maandalizi ya mechi ya robo fainali ya Kombe la FA (ASFC), itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Liti, mkoani Singida.

Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans Van Pluijim, amesema kambi hiyo imewasaidia kuwajenga wachezaji wake na amepata nafasi ya kucheza mechi mbili za kirafiki.

"Tumekaa kambini kwa siku nane, nadhani sasa zinatosha kabisa kuivaa Mbeya City, tumecheza na mechi mbili za kirafiki ambazo zimetupa changamoto ya kutosha kuwarudisha wachezaji kwenye hali ya ushindani," alisema Pluijm.

Naye meneja wa timu hiyo, Nizar Khalfan, alisema waliitaji kujiimarisha kwa sababu watakutana na timu inayowapa ushindani kila wanapocheza.

"Tunawajua Mbeya City, siyo timu mbaya, tumecheza nao kwenye ligi, hatukuwa na mechi nyepesi nao, tunahitaji kusonga mbele ili tuchukue ubingwa wa FA," alisema kiungo huyo wa zamani wa Yanga na Taifa Stars.

## Namungo, Ndanda FC kujipima makali

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuhakikisha inajiweka imara, Namungo inatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Ndanda FC itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani Lindi.

Namungo inatumia mchezo huo kujiwinda na mchezo wake wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbeya City utakaofanyika Aprili 9, mwaka huu.



Kocha Mkuu wa Namungo, Denis Kitambi (pichani), alisema lengo la mchezo huo ni kuwarejesha mchezoni nyota wake ambao wametoka katika mapumziko ya kalenda ya kimataifa.

"Kesho (leo) saa 2:00 usiku tunatarajia kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Ndanda, ninahitaji kuwaweka sawa na tayari wachezaji wangu kuelekea lala salama," alisema Kitambi.

Kocha huyo alisema baada ya mchezo huenda wakapata mechi nyingine ya kirafiki kwa sababu anahitaji kuwa na nyota wenye uwezo wa kupambana kupata matokeo chanya kwenye michezo iliyobakia msimu huu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### UNITED YAKOMAA NA KANE

MANCHESTER United inajiandaa kutoa dau la pauni milioni 80 ili kumnunua mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na Timu ya Taifa ya England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29, baada ya Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Richard Arnold, kuidhinisha mpango huo. ***(Star)***

### MOUNT ANUKIA BAYERN

BAYERN Munich inataka kumsajili kiungo wa kati wa Chelsea na Timu ya Taifa England, Mason Mount, mwenye umri wa miaka 24. ***(Times)***

### RASHFORD MAMBO BADO

MANCHESTER United haijachukua "hatua zozote zaidi" katika kuafiki mkataba mpya kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 25. ***(Athletic )***

### CITY YAMSUBIRI GUNDOGAN

KLABU ya Manchester City bado inamngoja kiungo wa kati wa Ujerumani, Ilkay Gundogan, kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wake, huku Barcelona wakitamani kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kwa uhamisho wa bure. ***(Fabrizio Romano)***

### BELLINGHAM ATAJWA CITY

IWAPO Ilkay Gundogan ataondoka Manchester City inamfikiria kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19, na kiungo wa kati wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Florian Wirtz (19), kama wachezaji wanaoweza kuchukua nafasi yake. ***(Football Insider)***

### ZERBI KUITAJIRISHA ITALIA

KLABU zinazovutiwa na Roberto de Zerbi zitalazimika kulipa kiasi fulani kwa Brighton kwa ajili ya kocha huyo wa Timu ya Taifa ya Italia, na makubaliano yanaweza tu kufanywa katika majira ya joto, si wakati wa huu msimu ukiendelea. ***(Fabrizio Romano)***

### KOVACIC, CHELSEA KUTETA

KLABU ya Chelsea bado haijaanza mazungumzo ya mkataba mpya na kiungo wa kati wa Croatia, Mateo Kovacic, huku Manchester City wakimtaka. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 amebakiza miezi 16 katika mkataba wake wa sasa. ***(Standard)***

### MIN-JAE ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL iko tayari kulipa zaidi ya pauni milioni 60 kumnunua beki wa kati wa Napoli na Timu ya Taifa ya Korea Kusini, Kim Min-jae, mwenye umri wa miaka 26, ambaye anasakwa na Manchester United. ***(Rai, via Four Four Two)***

### LINDSTROM ATAJWA ARSENAL

ARSENAL imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Denmark, Jesper Lindstrom, mwenye umri wa miaka 23, ambaye Eintracht Frankfurt itamruhusu kuondoka kwa ada ya takriban euro milioni 30. ***(Sport 1)***

### JAMES KUTUA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imefikia makubaliano ya awali ya mkataba wa kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Herbie James, mwenye umri wa miaka 16, kwa mkataba wa miaka mitatu kutoka akademi ya Manchester City. ***(Football London)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI AFUNGA MABAO 100 KWA ARGENTINA

**SANTIAGO DEL ESTERO,** Argentina

● ● ● Nyota huyo afikisha hat-trick ya tisa katika nchi yake huku pia akiwa...

LIONEL Messi anatumaini "furaha isiyokifani haitaisha" baada ya kufunga bao lake la 100 na hat-trick ya tisa kwa nchi yake katika mechi iliyochezwa juzi wakati Argentina ikiendelea kusherehekea taji la Kombe la Dunia.

**La Albiceleste waliibuka na ushindi wa mabao 7-0 dhidi ya Curacao mjini Santiago del Estero, huku bao la kwanza la Messi la dakika ya 20 likimfanya afikishe bao la 100 la kimataifa, akiungana na Cristiano Ronaldo (122) na Ali Daei (109) pekee kufanikisha hilo.**

Messi alifunga bao lake la 100 la kimataifa na hakuonyesha dalili zozote za kufikia mwisho kwani alifunga mabao mengine mawili kipindi cha kwanza na kumfanya afikishe jumla ya magoli 102 kwa Argentina.

Hatua hiyo muhimu ilikuja wakati Argentina ilipokamilisha mechi zake mbili za kwanza za kirafiki baada ya ushindi wa Kombe la Dunia, ikianza kuwafunga mabao 2-0 Panama mjini Buenos Aires, Alhamisi iliyopita.

Wachezaji hao waliiga sherehe zao kutoka Qatar baada ya mchezo wa Curacao, wakinyanyua tena Kombe la Dunia baada ya kushuka kutoka katika jukwaa la uwanja kwa heshima ya kuwasalimia mashabiki.

Messi pia alikabidhiwa bango na Rais wa Chama cha Soka cha Argentina (AFA) Claudio Tapia, kutambua bao lake la 100.

"Ni njia nzuri ya kufunga leo (juzi) kwa watu wote wa Santiago del Estero," aliandika Messi kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Natamani tuendelee kushiriki pamoja nyakati nyingi kama hizi na furaha hii haitaisha."

Mafanikio hayo ya Messi yanakuja baada ya kuanza kuifungia Argentina mabao 21 katika mechi 14 tu za kwanza tangu aanze kuichezea pamoja na asisti saba.


Hilo limemfikisha kwenye michango 156 ya mabao, ambayo ni mengi zaidi katika soka la kimataifa.

Kocha Mkuu wa Argentina, Lionel Scaloni, aliongeza: "Kuhusu Lionel Messi, ninachotaka ni awe uwanjani na kuwa na furaha."

Aliongeza: "Siku hizi zilikuwa tofauti na mechi za kirafiki za awali kwa sababu wachezaji waliruhusiwa kuwa na watu wao."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,096,0
MECHI KALI
SMOUHA CLUB
VERSUS
ISMAILY SC
1 | 2.61
X | 2.76
2 | 2.96
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ARTETA: SAKA ANA NAFASI KUBORESHA KIWANGO



**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amemsifu Bukayo Saka kwa uthabiti wake lakini anadai nyota huyo bado ana nafasi ya kuimarika.

Saka amekuwa nguzo muhimu katika mafanikio ya Ligi Kuu England kwa Arsenal msimu huu, huku timu hiyo ikiwa inaongoza kwa pointi nane mbele ya Manchester City inayoshika nafasi ya pili huku ikisaka taji lao la kwanza la ligi tangu msimu wa 2003-04.

Ni Erling Haaland wa Manchester City pekee na Harry Kane wa Tottenham Hotspur ndio walio na mabao mengi zaidi na wametoa pasi za magoli katika ligi msimu huu, huku Saka akiwa amefunga mabao 12 na asisti 10. Saka pia ameanza mechi zote 28 za ligi hiyo.

"Kwanza kabisa, nadhani lazima utambue kile ambacho amekuwa akifanya," alisema Arteta akiambia Sky Sports kuhusu Saka mwenye umri wa miaka 21.

"Uthabiti alioonyesha katika umri wake na kiwango hiki ni kitu cha nadra kuonekana.

"Ukiniuliza kama ana nafasi ya kuboresha, ningesema: 'Ndiyo - sana.' Hatosheki kamwe, huwa anataka zaidi na bado anaweza kufanya mambo mengi bora na kwa ufanisi zaidi, lakini tunafurahi sana kuwa naye."

Mazungumzo yanaendelea kati ya Arsenal na Saka kuhusu mkataba mpya, na mkataba wake wa sasa unatarajiwa kumalizika 2024.



## Son: Ninastahili kuwajibika

**SELOU,** Korea Kusini

HEUNG-Min Son anahisi "anawajibika" kwa Antonio Conte kuondoka Tottenham Hotspur kwa sababu ya kiwango chake kisichovutia uwanjani.

Conte aliondoka Spurs baada ya wiki ya uvumi mkubwa ukisema siku zake zimehesabika kutokana na kiwango kisichovutia.

Mechi ya mwisho ilikuwa ya sare mabao 3-3 dhidi ya Southampton, wakati Spurs iliongoza kwa magoli 3-1 kabla ya kuanguka kwa dakika za lala salama na hasira ya Conte baada ya mechi iliwaendea wachezaji wake kwa kuwaita "wabinafsi".

Conte pia alionekana kulenga ukosoaji wa uongozi wa klabu wakati wa maneno yake lakini inasemekana alifafanua siku chache baadaye maoni yote yaliwalenga wachezaji.

Hata hivyo, waaj
wake walionekana ku
mua uhusiano kati y
Conte na klabu hiy
umefikia pabaya, na t
laka ya "makubaliano y
pande zote" ilitangazwa

Son, akizungumza k
tika majukumu ya kim
taifa, alihisi kulaumiv
kwa kiasi fulani, huk
kiwango cha mcheza
huyo wa kimataifa w
Korea Kusini kikiv
kimeshuka kwa kiasi k
kubwa msimu huu.

041,286/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/04/23 | 17:00 | AFC Bournemouth vs Fulham FC | 2.45 | 3.10 | 2.80 |
| 02. 01/04/23 | 17:00 | Crystal Palace vs Leicester City | 2.46 | 3.10 | 2.75 |
| 03. 01/04/23 | 17:00 | Nottingham Forest vs Wolverhampton Wanderers | 2.85 | 3.00 | 2.45 |
| 04. 01/04/23 | 19:30 | Cadiz CF vs Sevilla FC | 3.05 | 3.00 | 2.33 |
| 05. 01/04/23 | 21:00 | SC Cambuur vs FC Emmen | 2.30 | 3.15 | 2.95 |
| 06. 01/04/23 | 22:00 | RKC Waalwijk vs Vitesse Arnhem | 2.55 | 3.25 | 2.60 |
| 07. 01/04/23 | 22:00 | Stade Rennes vs RC Lens | 2.36 | 3.25 | 2.80 |
| 08. 02/04/23 | 13:30 | Bologna FC vs Udinese Calcio | 2.23 | 3.15 | 3.10 |
| 09. 02/04/23 | 13:30 | Umraniyespor vs Konyaspor | 2.90 | 3.50 | 2.24 |
| 10. 02/04/23 | 15:15 | Grasshopper Club Zurich vs FC Lugano | 2.47 | 3.15 | 2.41 |
| 11. 02/04/23 | 16:00 | FC Nantes vs Stade Reims | 2.90 | 3.20 | 2.33 |
| 12. 02/04/23 | 16:00 | Stade Brest 29 vs Toulouse FC | 2.80 | 3.30 | 2.34 |
| 13. 02/04/23 | 16:00 | Giresunspor vs Alanyaspor | 2.33 | 3.20 | 2.50 |
| 14. 02/04/23 | 17:30 | Maritimo Madeira vs Boavista Porto | 2.55 | 3.10 | 2.70 |
| 15. 02/04/23 | 18:30 | Newcastle United vs Manchester United | 2.39 | 3.20 | 2.80 |
| 16. 02/04/23 | 18:30 | Werder Bremen vs TSG Hoffenheim | 2.23 | 3.45 | 2.85 |
| 17. 02/04/23 | 19:30 | Villarreal CF vs Real Sociedad San Sebastian | 2.28 | 3.05 | 3.10 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 30/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1140 | Chuncheon FC vs Paju Citizen FC | 4.46 | 3.57 | 1.68 |
| 13:00 | 3281 | Daejeon Korail vs Sangju Sangmu | 9.92 | 5.58 | 1.22 |
| 13:00 | 4016 | Busan Transp. vs Dangjin Citizen | 1.59 | 3.73 | 4.97 |
| 13:00 | 4129 | Gangneung City vs Gyeongnam | 5.39 | 4.25 | 1.47 |
| 13:00 | 4580 | Gyeongju KHNP vs Geoje Citizen | 1.40 | 4.75 | 5.79 |
| 13:00 | 4956 | Cheonan City FC vs Yangju Citizen FC | 2.07 | 3.05 | 3.46 |
| 14:00 | 2029 | Bursaspor vs Bayburt Idare | 1.54 | 3.79 | 5.40 |
| 16:30 | 3576 | Dewa United vs Persik Kediri | 2.35 | 3.14 | 2.73 |
| 16:30 | 4618 | Bhayangkara Surabaya Utd vs Rans Nusantara | 1.38 | 4.42 | 6.37 |
| 17:00 | 1802 | Atletico Tucuman Reserve vs Colon de Santa Fe Reserve | 2.55 | 2.90 | 2.49 |
| 17:00 | 2696 | Newells Old Boys vs Estudiantes de LP Reserve | 2.64 | 3.00 | 2.58 |
| 17:00 | 4292 | CA Platense vs Banfield Reserve | 2.79 | 2.95 | 2.48 |
| 17:00 | 4421 | Erzurum BB vs Altay | 1.80 | 3.39 | 3.86 |
| 17:00 | 5726 | Velez Sarsfield Reserve vs Defensa Y Justicia Reserve | 2.05 | 3.16 | 3.37 |
| 18:30 | 2492 | Sanat Mes Kerman FC vs Aluminium Arak | 3.11 | 2.50 | 2.64 |
| 18:45 | 1805 | Naft Masjed Soleyman FC vs Teraktor Sazi | 4.27 | 3.07 | 1.85 |
| 18:45 | 5721 | Malavan Bandar Anzali vs Havadar | 2.60 | 2.61 | 3.02 |
| 19:00 | 2461 | Peykan FC vs Foolad Khuzestan | 3.26 | 2.64 | 2.42 |
| 19:00 | 5453 | Esteghlal Mollasani vs Shahrdari Hamedan | 2.12 | 2.70 | 3.89 |
| 19:45 | 4040 | Wolfsburg W vs Paris Saint Germain W | 1.76 | 3.78 | 3.73 |
| 20:00 | 3903 | FC Otelul Galati vs CSA Steaua Bucuresti | 2.63 | 2.93 | 2.57 |
| 20:30 | 3122 | Sakaryaspor vs Eyupspor | 3.03 | 3.34 | 2.08 |
| 21:00 | 3141 | America MG U20 vs Fluminense RJ U20 | 1.80 | 3.25 | 3.60 |
| 21:00 | 4564 | AL Tawon SC vs Emirates Club | 4.81 | 3.99 | 1.53 |
| 21:45 | 1147 | Etehad Alreef vs Malkiya Club | 6.22 | 4.35 | 1.41 |
| 21:45 | 5123 | Najma Manama vs Bouri | 1.50 | 4.05 | 5.40 |
| 21:45 | 5814 | Qalali vs Um Alhassam | 2.25 | 2.90 | 3.21 |
| 22:00 | 2045 | Chelsea W vs Lyon W | 2.58 | 3.58 | 2.30 |
| 22:15 | 2636 | Smouha Club vs Ismaily SC | 2.61 | 2.76 | 2.96 |
| 22:15 | 3186 | Ceramica Cleopatra vs Arab Contractors | 2.49 | 2.80 | 3.05 |
| 22:15 | 5013 | Enppi Club vs National Bank | 2.77 | 2.87 | 2.67 |

IJUMAA - 31/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 19:30 | 3259 | Fortuna Dusseldorf vs Hamburger SV | 2.40 | 3.64 | 2.58 |
| 19:30 | 4017 | Nurnberg vs SV Darmstadt | 3.23 | 3.34 | 2.12 |
| 19:30 | 5885 | FC Fredericia vs Nykobing FC | 1.72 | 3.65 | 3.95 |
| 20:00 | 1942 | Odense vs Midtjylland | 2.98 | 3.48 | 2.21 |
| 21:00 | 1336 | PEC Zwolle vs Jong Utrecht | 1.16 | 6.67 | 12.50 |
| 21:00 | 1544 | VVV Venlo vs NAC Breda | 1.89 | 3.44 | 3.65 |
| 21:00 | 2667 | Maastricht vs FC Eindhoven | 2.76 | 3.44 | 2.26 |
| 21:00 | 2849 | ADO Den Haag vs Telstar | 2.05 | 3.38 | 3.22 |
| 21:30 | 3103 | Eintracht Frankfurt vs VfL Bochum | 1.52 | 4.09 | 5.39 |
| 21:30 | 3218 | Genoa vs Reggina | 1.65 | 3.46 | 5.14 |
| 21:45 | 5912 | Zulte Waregem vs Royal Antwerp | 4.02 | 3.82 | 1.74 |
| 22:00 | 2421 | Levante vs Zaragoza | 1.73 | 3.29 | 4.78 |
| 22:00 | 3592 | Marseille vs Montpellier | 1.42 | 4.41 | 6.22 |
| 22:00 | 4859 | Burnley vs Sunderland | 1.46 | 4.20 | 6.00 |
| 22:00 | 5773 | Mallorca vs Osasuna | 2.19 | 2.80 | 3.60 |
| 22:15 | 3486 | Ghazl EL Mahallah vs El Ittihad Alexandria | 3.31 | 3.00 | 2.22 |
| 22:15 | 4349 | GD Estoril vs Gil Vicente | 2.66 | 3.21 | 2.51 |
| 22:15 | 5799 | Farco FC vs Aswan | 2.31 | 2.86 | 3.31 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# NAMUNGO YAANDAA DARASA MAALUM KWA WALINZI WAKE

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Namungo, Denis Kitambi, amesema jukumu lake kubwa kwa sasa ni kuimarisha safu ya ulinzi ambayo imeruhusu mabao mepesi katika mechi mbalimbali walizocheza baada ya kukiri walishaondoka kwenye mbio za kusaka ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kitambi aliliambia gazeti hili anajiandaa kuifumua na kuisuka upya safu hiyo ili iwe imara baada ya kubaini mapungufu katika mechi tatu zilizopita.

"Tumerejea mazoezini, tumeanza na mazoezi ya utimamu wa mwili, lakini kadri siku zinavyokwenda mbele, nitafanya programu maalumu itakayosaidia kumaliza mapungufu hayo, au kupunguza idadi ya mabao tunayoruhusu, hiki ndiyo chanzo kikubwa cha kupoteza mechi zetu tatu zilizopita," alisema Kitambi.

**Naye nahodha wa timu hiyo, Hamisi Mgunya, amesema lengo lao msimu huu ni kubakia katika Ligi Kuu Tanzania Bara na kumaliza msimu kwa kushinda mechi zilizobaki.**

"Ligi ni ngumu na hakuna timu iliyo tayari kushuka, na inavyoonekana usipofanya vizuri kuna hatari kubwa mwenzako akakupita, kwa hiyo sisi tunachoangalia ni kushinda mechi zetu na siyo kuangalia aliye juu yetu wala chini yetu," alisema mchezaji huyo.

Namungo imetolewa katika michuano ya Kombe la FA, imekuwa na mwendo wa kusuasua kutokana na kuyumba kwa kikosi chao.

Mechi yake ya mwisho ya Ligi Kuu, ilikubali kipigo cha mabao 3-2 kutoka kwa Prisons ya Mbeya na katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara iko katika nafasi ya nane ikiwa na pointi 32.



Aliyekuwa Rais wa Chama cha Gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU), Sophia Viggo (wa tatu kushoto), akimkabidhi katiba ya chama hicho rais mpya, Queen Siraki (wa tatu kulia), baada ya kushinda katika uchaguzi mkuu uliofanyika wikendi iliyopita. Wanaoshuhudia zoezi hilo ni viongozi wapya wa TLGU waliopatikana katika uchaguzi huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Stars matumaini AFCON

INATOKA UKURASA 24

sana kwa Uganda ambayo kwa sasa ipo katika kipindi cha mpito wa mabadiliko wa kujaribu kuingiza wachezaji vijana wanaoshirikiana na nyota wachache wazoefu.

"Tunarekodi nzuri ya kuwatoa Tanzania katika michuano mbalimbali ikiwamo CHAN, hilo sikutaka kubadili mtazamo wangu na mabadiliko tuliyoyafanya ya kiufundi yametusaidia kupata ushindi," alisema Micho.

Aliongeza anaimani uwanja wao wa nyumbani (Namboole) utakuwa tayari kwa kutumia katika mechi dhidi ya Niger na wamekuwa na matokeo mazuri wanapocheza hapo.

"Ni kundi ngumu sana, tunatakiwa kupambana kwa sababu ya aina ya msimamo ulivyo, Uganda na Tanzania, tuko sawa kwa pointi na hata mabao ya kushinda, sasa huu ni muda wa kila mmoja kupambana katika michezo yake ili kufanikiwa kusonga mbele," Micho alisema.

## *Simba, Yanga kazi iendelee*

INATOKA UKURASA 24

fainali," alisema Nabi.

Aliongeza hatua waliyofika ni ngumu zaidi na mechi dhidi ya TP Mazembe ni muhimu ili kuwaandaa wachezaji wake na hatua ya mtoano ambayo wanaelekea.


"Tunakwenda kutafuta matokeo chanya licha ya kutambua mchezo huo utakuwa mgumu, washambuliaji wanatakiwa kuwa makini na kuhakikisha hawapotezi nafasi wanazotengeneza ili kutafuta ushindi, kila mchezaji anatakiwa kujiimarisha na kutumia mechi hii kujiweka tayari na vita iliyoko mbele yetu," aliongeza kocha huyo.

Aliongeza wachezaji wote waliokuwa katika kikosi cha Timu ya Tanzania (Taifa Stars), wamesharejea kambini isipokuwa kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto', ambaye bado ameendelea na msimamo wake wa kutohitaji kurejea ndani ya timu hiyo.

# Michezo

Alhamisi Machi 30, 2023

Nipashe

Messi afunga mabao 100 kwa Argentina UKURASA 21



Beki wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr' (kushoto), akijiandaa kumtoka mchezaji wa Uganda katika mechi ya Kundi F ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023) iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi usiku. Stars ililala bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## Stars matumaini AFCON palepale

**Na Saada Akida**

BEKI wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Novatus Dismas, amesema licha ya kupoteza nyumbani dhidi ya Uganda (The Cranes), bado wana nafasi ya kupata tiketi ya kucheza Fainali za Kombe la Afrika (AFCON) kwa kutafuta matokeo chanya katika mechi zilizobakia.

Stars ilihitaji pointi tatu ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele kabla ya kushuka dimbani katika mechi mbili zilizobakia lakini ilipoteza bao 1-0 kwa majirani zao hao Uganda.

Stars sasa itasubiri kupata ushindi katika mechi inayofuata dhidi ya Niger itakayochezwa Juni 12, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili baada ya kukamilika kwa dakika 90 kukamilika, Novatus alisema hakuna anayepaswa kulaumiwa kwa matokeo hayo na wanatakiwa kujipanga kwa ajili ya mechi ijayo.

Beki huyo alisema mechi ilikuwa ngumu na makosa madogo waliyofanya yaliwapa Uganda nafasi ya kupata bao pekee la ushindi.

"Watanzania wote wameona mechi ilikuwa ngumu, tulifanya makosa madogo dakika za mwisho na wapinzani wetu kuyatumia, hakuna na kumlaumu wala kumwonyeshea kidole mtu. Maneno mabaya hayawezi kutujenga, kikubwa Watanzania waendelee kutusapoti na kutuunga mkono tuweze kufanya vizuri mchezo wetu wa mwisho," alisema nyota huyo anacheza soka la kulipwa katika klabu ya Zulte Waregem inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza huko Ubelgiji.

Naye Kocha wa The Cranes, Milutin Sredojovic 'Micho', aliwapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo muhimu.

Micho alisema ushindi huo una maana kubwa

INAENDELEA UKURASA 23

# Simba, Yanga kazi iendelee

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

### ●●● Makocha watamba wanafuata ushindi kwa ajili ya kujiimarisha kuelekea...

WAKATI kikosi cha Yanga kinatarajia kuondoka nchini leo kuelekea Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), kuwafuata TP Mazembe, kundi la kwanza la Wekundu wa Msimbazi limewasili Morocco tayari kuwakabili wenyeji Raja Casablanca.

**Hata hivyo kikosi cha Simba kilichokuwa na wachezaji 13, benchi la ufundi na viongozi juzi kilikwama kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mkoa wa Kilimanjaro (KIA), baada ya ndege waliokuwa wakisafiria kupata hitilafu na hivyo walilazimika kulala jijini, Arusha.**

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema ndege waliyokuwa wakisafiria ilipata hitilafu na walitaarifiwa safari haitaendelea.

Kundi la pili la wachezaji wa timu hiyo ambayo walikuwa katika majukumu ya kimataifa lilitarajiwa kuwasili Morocco kwa nyakati tofauti leo kwa ajili ya mechi ya mwisho ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kwenye Uwanja wa Momamed V usiku wa kuamkia Jumamosi.

Vinara wa Kundi C, Raja Casablanda yenye pointi 13 na Simba inayofuata yenye pointi tisa, zimeshasonga mbele katika michuano hiyo.

Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho' amesema pamoja na kutinga robo fainali, lakini wanakwenda kupambana kwa ajili ya kusaka ushindi na kukiweka sawa kikosi chake kuelekea hatua inayofuata.

"Tuko katika kiwango kizuri sasa kuliko mwanzo tulipokutana nao, hivi sasa wachezaji wangu wapo moto, kuna Kibu Denis, kuna kiwango bora cha Jean Baleke, halafu nyuma hapa nina, Clatous Chama na Saido Ntobazonkiza, wote wapo kwenye kiwango cha juu kuliko mwanzo tulipokutana nao, tunaweza kabisa kulipa kisasi, " alisema Robertino.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ameliambia gazeti hili yuko tayari kukutana na timu yoyote katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika na sasa wanaenda kusaka ushindi ili kumaliza kileleni katika kundi lao.

Kocha huyo alisema wana kazi kubwa ya kufanya katika mechi yao dhidi ya TP Mazembe lakini hawana hofu kutokana na uimara wa wachezaji wake kwa sasa.

Alisema kazi kubwa anayoifanya ni kuwasisitiza wachezaji wake kuongeza umakini wa kutumia vyema nafasi wanazotengeneza na hiyo itawasaidia katika mechi muhimu ya hatua ya robo fainali.

"Ni kweli tayari tumetinga robo fainali huku tukiwa na mechi moja mkononi dhidi ya TP Mazembe, mchezo utakuwa mgumu, tunahitaji kupata pointi tatu ili tuongoze kundi, lakini tuko tayari kukutana na timu yoyote ambayo tutapangwa nayo katika hatua inayofuata ya robo

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >